

**KUTATHIMINI MATUMIZI YA LUGHA NA DHAMIRA KATIKA
TAMTHILIA ZA KINJEKETILE NA NYERERE NA SAFARI YA
KANAANI: UTAFITI LINGANISHI**

CYPRIAN FIDES

**TASNIFU ILIYOWASILSHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A KISWAHILI) YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2017

UTHIBISHO

Aliyetia sahihi hapa anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo, **Kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya za Kinjeketile na Nyerere na Safari ya Kanaani: Utafiti linganishi** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kwa ajili kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili (M.A) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Prof. Emmanuel D. Y. Mbogo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, kubadilishwa kwa mbinu yoyote ile: kieletroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi, **Cyprian Fides**, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu, familia yangu, walimu na wanafunzi wenzangu ambao wamejitoa kwa hali na mali katika kufanikisha malengo yangu ya kitaaluma ambayo yamenifikisha hatua hii ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili.

SHUKURANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, nguvu na uwezo wa kukamilisha kazi hii. Nawashukuru wote waliokuwa wakinipa ushauri na mawazo mbalimbali hasa walimu wangu wa shahada ya uzamili. Ni vigumu kuwataja wote ila sina budi kuwaomba radhi wale nisiowataja. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Profesa Emmanuel D. Y. Mbogo ambaye hakusita wala kuchoka kunishauri katika hatua zote za ukamilishaji wa kazi hii. Kwa hakika alijitoa sana katika kuniongoza, kunishauri, kunikosoa na kunielekeza katika hatua mbalimbali za utafiti wangu. Hivyo kutokana na ushauri wake ilinilazimu kutumia muda mwangi kutafakari na kufanya kazi maelekezo yake yалиyonisaidia kukamilisha utafiti huu. Nakushukuru sana Profesa Mbogo, nakuombea kwa Mungu akupe maisha marefu yenye baraka, amani na furaha tele. Pia napenda kuwashukuru wazazi wangu wapendwa, Bwana Cyprian Abel Moshy na Bi Josephine Jacob Tengia kwa kenisomesha hatua mbalimbali hadi kufikia kusoma Shahada ya Uzamili. Mungu awabariki awape afya, amani na furaha katika maisha yenu yote.

Aidha napenda kumshukuru mume wangu mpendwa Bwana Sixbert John Mahundi kwa kunipa msaada wa hali na mali na kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Pia nawashukuru watoto wangu Alice, Stanley na Charles kwa kunipa ushirikiano katika kusoma kwangu na kuniwezesha kukumilisha kazi hii ya uzamili. Vilevile nawashukuru wanachuo wenzangu wa shahada ya uzamili, kwa ushirikiano walionipa kwa kunihimiza na kunitia moyo bila kuchoka ili niweze kumaliza shahada yangu ya uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani: Utafiti linganishi*. Ili kufanikisha utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu za maktabani katika kukusanya na kuwasilisha data kimaelezo. Pia marejeleo mbalimbali kutoka tamthiliya za Kiswahili yalipitiwa. Nadharia ya fasihi ya jamii ndiyo iliyotumika katika kufanikisha utafiti huu. Nadharia hii imemsaidia mtafiti kuweza kubaini mawazo mbalimbali ya waandishi katika tamthiliya zao za utafiti linganishi. Matokeo ya uchanganuzi wa data yaliweza kujibu maswali ya utafiti. Tamthiliya hizi teule zimebainisha jamii yetu kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Dhamira za uongozi mbaya, rushwa na usaliti zimejitokeza. Matokeo mengine ni dhamira ya ukombozi iliyomfanya mkoloni aondolewe katika ardhi ya jamii ya watu wa Kusini ili wawe huru, kutumia ardhi yao na mali nyingine zilizopatikana katika jamii yao. Pia uzalendo ultakiwa kwa jamii kwa kuwapeleka vijana kwenye mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na tohara. Tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani* zina mchango mkubwa katika jamii kwa kuwasilisha ujumbe ambao ni wa kihistoria unaoiwezesha kujua matukio mbalimbali ya nchi kabla na baada ya uhuru

YALIYOMO

| | |
|---|-------------|
| UTHIBISHO..... | ii |
| HAKIMILIKI..... | iii |
| TAMKO | iv |
| TABARUKU..... | v |
| SHUKURANI | vi |
| IKISIRI | vii |
| ORODHA YA MAJEDWALI..... | xiii |
| SURA YA KWANZA..... | 1 |
| UTANGULIZI..... | 1 |
| 1.1 Utangulizi | 1 |
| 1.2 Usuli wa Mada | 2 |
| 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti | 4 |
| 1.4 Malengo ya Utafiti | 5 |
| 1.4.1 Lengo Kuu..... | 5 |
| 1.5 Maswali ya Utafiti | 5 |
| 1.6 Umuhimu wa Utafiti..... | 6 |
| 1.7 Mipaka ya Utafiti | 6 |
| 1.8 Uzingativu wa Maadili | 6 |
| 1.9 Vikwazo vya Utafiti | 7 |
| 1.10 Utatuzi wa Vikwazo | 7 |
| 1.11 Muundo wa Tasnifu | 8 |
| 1.12 Hitimisho..... | 8 |

| | |
|---|-----------|
| SURA YA PILI..... | 9 |
| MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA | 9 |
| 2.1 Utangulizi | 9 |
| 2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi..... | 9 |
| 2.3 Tafiti kuhusu Tamthiliya za Kiswahili | 11 |
| 2.4 Pengo la Utafiti | 14 |
| 2.5 Matumizi ya Lughा | 14 |
| 2.5.1 Tamathali za semi..... | 14 |
| 2.5.2 Kejeli | 16 |
| 2.5.3 Sitiari | 16 |
| 2.5.4 Tashihisi | 17 |
| 2.5.5 Tashibiha | 17 |
| 2.5.6 Takriri..... | 17 |
| 2.5.8 Tashtiti..... | 18 |
| 2.5.9 Mdokezo..... | 18 |
| 2.6 Dhana ya Dhamira..... | 19 |
| 2.7 Kiunzi cha Nadharia..... | 20 |
| 2.7.1 Nadharia ya fasihi ya jamii..... | 21 |
| 2.8 Hitimisho | 22 |
| SURA YA TATU..... | 23 |
| MBINU NA NJIA ZA UTAFITI..... | 23 |
| 3.1 Utangulizi..... | 23 |
| 3.2 Eneo la Utafiti | 23 |
| 3.3 Kundi Lengwa..... | 23 |

| | | |
|-------|---|-----------|
| 3.4 | Usampulishaji..... | 24 |
| 3.5 | Sampuli | 24 |
| 3.6 | Mbinu za ukusanyaji data..... | 24 |
| 3.6.1 | Mbinu ya Usomaji Matini mbalimbali | 24 |
| 3.7 | Zana za Utafiti..... | 25 |
| 3.7.1 | Matini | 25 |
| 3.7.2 | Kompyuta | 26 |
| 3.7.3 | Simu ya mkononi | 26 |
| 3.8 | Hitimisho | 26 |
| | SURA YA NNE..... | 27 |
| | UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA..... | 27 |
| 4.1 | Utangulizi..... | 27 |
| 4.2 | Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya Teule..... | 27 |
| 4.3 | Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya za <i>Kinjeketile na Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 28 |
| 4.4 | Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi | 29 |
| 4.4.2 | Nidaa | 31 |
| 4.4.3 | Tashibiha | 33 |
| 4.4.4 | Tashihisi | 34 |
| 4.4.5 | Sitiari | 35 |
| 4.4.6 | Takriri..... | 37 |
| 4.4.7 | Tashtiti..... | 38 |
| 4.4.8 | Tanakali Sauti..... | 39 |
| 4.4.9 | Kejeli | 40 |

| | | |
|--------|---|----|
| 4.4.10 | Mdokezo..... | 41 |
| 4.5 | Misemo..... | 42 |
| 4.6 | Methali | 44 |
| 4.7 | Nahau | 45 |
| 4.8 | Tamathali za Semi katika Tamtiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 46 |
| 4.8.1 | Nidaa | 47 |
| 4.8.2 | Takriri..... | 48 |
| 4.8.3 | Sitiari | 50 |
| 4.8.4 | Tashibiha | 51 |
| 4.8.5 | Kejeli | 52 |
| 4.8.6 | Tashtiti..... | 53 |
| 4.8.7 | Tashihisi | 54 |
| 4.8.8 | Mdokezo..... | 54 |
| 4.9 | Methali | 55 |
| 4.10 | Misemo..... | 56 |
| 4.11 | Kuwasilisha Dhamira kuu za Tamthiliya..... | 57 |
| 4.12 | Kulinganisha na Kulinganua Vipengele vya lugha katika Tamthiliya za <i>Kinjeketile na Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 59 |
| 4.13 | Kufanana | 59 |
| 4.14 | Kutofautiana | 61 |
| 4.15 | Kufanana au Kutofautiana kwa Dhamira Zilizojitokeza katika Tamthiliya Teule | 62 |
| 4.15.1 | Matabaka | 62 |
| 4.15.2 | Uongozi Mbaya | 63 |

| | |
|---|-----------|
| 4.15.3 Nafasi ya Mwanamke | 63 |
| 4.15.4 Umaskini | 64 |
| 4.15.5 Rushwa na Usaliti..... | 64 |
| 4.15.6 Mapenzi | 65 |
| 4.15.7 Ukombozi | 65 |
| 4.15.8 Hitimisho | 66 |
| SURA YA TANO | 67 |
| MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..... | 67 |
| 5.1 Utangulizi..... | 67 |
| 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti | 67 |
| 5.3 Hitimisho | 71 |
| 5.4 Mapendekezo | 73 |
| MAREJELEO | 74 |

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|---|----|
| Jedwali Na 4.1: Vipengele vya lugha katika <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 27 |
| Jedwali Na 4.2: Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 28 |
| Jedwali Na 4.3: Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> na <i>Nyerere na Safari yaKanaani</i> | 28 |
| Jedwali Na 4.4: Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya <i>Nyerere na Safari ya Kanani</i> | 30 |
| Jedwali Na 4.5: Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 30 |
| Jedwali Na 4.6: Mifano ya baadhi ya Nidaa katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 32 |
| Jedwali Na 4.7: Tashibiha katika Tamthiliya ya <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 33 |
| Jedwali Na 4.8: Baadhi yaTashihisi Zilizojitokeza katika Tamthilia ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari ya Kanaani</i> | 35 |
| Jedwali Na 4.9: Sitiari katika Tamthiya ya <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | 36 |
| Jedwali Na 4.10: Ujitokezaji wa Takriri katika Tamthiliya ya <i>Nyerere na</i> <i>Safari ya Kanaani</i> | 37 |
| Jedwali Na 4.11: Ujitokezaji wa Tashtiti katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari ya Kanaani</i> | 38 |
| Jedwali Na 4.12: Matumizi ya baadhi ya Tanakali Sauti katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 40 |
| Jedwali Na 4.13: Ujitokezaji wa Kejeli katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 41 |

| | |
|---|----|
| Jedwali Na 4.14: Ujitokezaji wa Mdokezo Katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 42 |
| Jedwali Na 4.15: Ujitokezaji wa Misemo katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 43 |
| Jedwali Na 4.16: Ujitokezaji wa Methali katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari yaKanaani</i> | 44 |
| Jedwali Na 4.17: Ujitokezaji wa Nahau katika Tamthiliya ya <i>Nyerere</i> na <i>Safari ya Kanaani</i> | 45 |
| Jedwali Na 4.18: Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 47 |
| Jedwali Na 4.19: Ujitokezaji wa Nidaa katika Tamthilia ya <i>Kinjeketile</i> | 48 |
| Jedwali Na 4.20: Ujitokezaji wa Takriri katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 49 |
| Jedwali Na 4.21: Ujitokezaji wa Sitiari katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 50 |
| Jedwali Na 4.22: Ujitokezaji wa Tashibiha katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 51 |
| Jedwali Na 4.23: Ujitokezaji wa Kejeli kutoka katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 52 |
| Jedwali Na 4.24: Ujitokezaji wa Tashititi katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 53 |
| Jedwali Na 4.25: Ujitokezaji wa tashihisi katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 54 |
| Jedwali Na 4. 26: Ujitokezaji wa Mdokezo katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 55 |
| Jedwali Na 4.27: Ujitokeazji wa Methali katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 56 |
| Jedwali Na 4.28: Ujitokezaji wa misemo katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 56 |
| Jedwali Na 4.29: Ujitokezaji wa Dhamira katika Tamthiliya Teule | 57 |
| Jedwali Na 4.30: Ujitokezaji wa Dhamira katika Tamthiliya ya <i>Kinjeketile</i> | 58 |
| Jedwali Na 4.31: Vipengele vya Luga Vinavyofanana katika Tamthiliya Teule ... | 60 |
| Jedwali Na 4.32: Vipengele vya Luga Vinavyotofautiana katika Tamthiliya | |

| | |
|---|----|
| Teule..... | 61 |
| Jedwali Na 4.33: Kufanana kwa Dhamira Zilizowasilishwa na Vipengele vya Lugha..... | 62 |
| Jedwali Na 4.34: Kutofautiana kwa Dhamira zilizowasilishwa na Vipengele vya Lugha..... | 64 |

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii tangulizi inatoa usuli wa mada katika utafiti huu. Sura hii inahusu usuli wa mada, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, uzingativu wa maadili, vikwazo vya utafiti, utatuzi wa vikwazo, muundo wa tasnifu na hitimisho. Kabla ya kuanza tupate historia fupi ya wasanii wa tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*. Tamthiliya ya *Kinjeketile* imetungwa na msanii Ebrahim Hussein (1969) ambaye ni msanii aliyeandika kazi hii ya kisanii kwa kutumia tukio la kihistoria lililotokea Kusini mwa Tanzania. Wananchi wa Kusini walipambana na Mjerumani ili kumwondoa katika ardhi yao. Mwandishi ameonesha jinsi wananchi walivyoamini kuwa maji ni kinga ya vita kwa kuwa itafanya risasi kuwa maji. *Kinjeketile* aliaminiwa na wananchi wa Kusini na kuweza kuwaunganisha makabila ya Kusini kuwa kitu kimoja na mshikamano na kupambana na Mjerumani. Mwandishi ameendelea kuonesha kuwa maji yalikuwa ni ishara ya umoja kwa kuwa kuitia imani ya maji wananchi waliweza kuungana na kupambana na Mjerumani. Msanii E. Hussein anafaa kuigwa kwa mchango wake katika fasihi ya Kiswahili.

Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* imetungwa na msanii Emmanuel Mbogo (2015) ambaye ameandika jambo la kihistoria baada ya Tanzania kupata uhuru. Msanii ametuonesha baada ya uhuru watu wachache walijilimbikizia mali kwa muda mfupi na kuwa matajiri. Hvyo watu hawa walikuwa wamepingana na Rais

Nyerere. Profesa E. Mbogo ni maarufu kwa uandishi wa Drama na Fasihi ya Kiswahili na mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

1.2 Usuli wa Mada

Katika fasihi yoyote ni lazima iwe na fani na maudhui. Katika fani kunakuwa na mtindo, lugha, mandhari, na wahusika. Wasanii wa kazi za tamthiliya wanapenda kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika kazi zao ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Kazi yoyote ya msanii ili iweze kueleweka vizuri lazima lugha ichambuliwe kufuatana na jinsi iliyotumika katika vipengele vyake mbalimbali kwa pamoja ili kuleta maana kamili iliyopo katika kazi hiyo. Kila msanii ana ubunifu wake katika kuandika kazi yake kwa kubuni mtindo atakaoutumia katika kazi yake kwa mfano katika kuteua msamati muundo na lugha. Katika kuchunguza kazi ya msanii ili kupata ujumbe wa kazi hiyo hatuna budi kuhusisha vipengele vya lugha katika kazi husika.

Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya lugha iliyotumika kulingana na vipengele vyake na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein na tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* iliyoandikwa na Profesa Emmanuel Mbogo. Katika kazi hii utafiti umetathmini matumizi ya lugha iliyotumika katika tamthiliya hizi ikiwa ni pamoja na vipengele vyake na dhamira zilizojitokeza katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii kwa kuwalinganisha na kuwatofautisha waandishi hawa wawili. Utafiti huu umekuwa wa kihistoria umetumia lugha kwa kuitia vipindi mbalimbali kuonesha mchango wa waandishi hawa katika kazi ya sanaa ya uandishi. Waandishi hawa wamechangia kukuza historia ya nchi yetu na kuiwezewesha jamii kuona umuhimu wa kusoma

tamthiliya za kihistoria ili kupata maarifa ya kihistoria yaliyopo na kuweza kuona nchi imetoka wapi.

Katika kutathmini matumizi ya lugha utafiti huu umewalinganisha wasanii wawili ambapo ni msanii E. Mbogo ambaye ni msanii nguli aliyebolea katika kuandika drama na kuielimisha jamii kupitia tamthiliya zake. Kwa utafiti huu tumetumia kitabu chake cha *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) ambapo ameelezea Nyerere na harakati za kuimarisha vijana kabla ya kuanza kazi wawe wazalendo kwa kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa. Vilevile kuwawezesha vijana kujitegemea hata pale ambapo hawatapata ajira. Tumefanya utafiti pia kwa kutumia tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyotungwa na msanii Ebrahim Hussein ambaye katika uandishi naye pia anaibua hisia za usomaji kwa kuandika tamthiliya za Kiswahili. Mwandishi anaonesha Kinjeketile alivyokuwa akiwaunganisha wananchi wa Kusini wakati wakipambana na Wajerumani akitetea uhuru wa Waafrika, akilaani uonevu wa wakoloni kwa Waafrika katika nchi yao kwa kubaguliwa na kutengwa kabisa na wazungu (Wajerumani). Kinjeketile alionesha maji yalivytumiwa kama kinga dhidi ya mashambulizi ya risasi zilizokuwa zikipigwa na Wajerumani. Kinjeketile alitumia maji kwa kuwaunganisha wananchi kuwa kitu kimoja ili waweze kumshambulia Mjerumani kwa urahisi. Na alifanikiwa kuyaunganisha makabila ya Kusini mwa Tanzania na kuwa na imani kuwa watamshinda Mjerumani.

Tamthiliya hizi za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* ni tamthiliya za kihistoria kwa kuwa zinawazungumzia watu au wanaharakati wa kihistoria katika nchi yao waliokuwa wakitetea wanachi kutoka katika makucha ya wakoloni. Wanaharakati hawa walikuwa na uchungu na nchi yao kwa uzalendo

waliokuwa nao bila woga walitetea waziwazi uhuru wa nchi yao. Kupitia tamthiliya hizi jamii imejifunza jinsi nchi zilivyopitia misukosuko katika kuleta mabadiliko katika nchi yao.

Kupitia kwa wasanii hawa jamii imeendelea kujifunza historia ya nchi kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kuwa historia hubaki kuwa historia wakati wote. Hivyo wasanii huchangia kwa kiasi kikubwa muendelezo wa matukio mbalimbali ambayo yatabaki kuwa ni historia. Utafiti huu umechunguza na kutathmini matumizi ya lugha na dhamira ikiwa ni pamoja na vipengele vya lugha kwa kulinganisha tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaan*. Aidha umechunguza kutofautiana au kufanana kwa wasanii hawa katika kufikisha ujumbe kwa jamii.

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Katika kuelezea jambo la kihistoria katika jamii waandishi wa kazi za sanaa wanaweza kutumia lugha kufikisha ujumbe uliokusudiwa kuwezesha kizazi kimoja hadi kingine kujifunza historia. Waandishi wa wana jukumu la kutumia lugha inayomwezesha msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa.

Tatizo la utafiti ni kwamba tamthiliya za kihistoria hazijafanyiwa uchunguzi wa kina na kuweka wazi jinsi lugha na vipengele vyake vinavyoweza kumtofautisha na kumfananisha msanii mmoja na mwingine katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Kwa utafiti huu tutaweza kuainisha matumizi ya lugha na dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya teule. Pia kulinganisha na kulinganua matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya hizo.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umetathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya za *Kinjeketile* (1970) na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) katika kuwasilisha kwa namna tofauti ujumbe uliokusudiwa kwa jamii.

1.4.1 Lengo Kuu

Kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya teule ili kubaini vipengele vinavyotofautiana na vinavyofanana katika kutumia lugha kufikisha ujumbe katika mkabala wa fasihi linganishi.

1.4.2 Malengo Mahsusini

Utafiti huu una malengo mahsusini yafuatayo:

- (i) Kuainisha vipengele vya lugha katika tamthiliya teule.
- (ii) Kulinganisha na kulinganua vipengele vya lugha katika tamthiliya teule kufikisha.
- (iii) Kuainisha dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya teule.
- (iv) Kulinganisha na kulinganua dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya teule.

1.5 Maswali ya Utafiti

- (i) Ni vipengele vyi vya lugha vinajitokeza katika tamthiliya teule?
- (ii) Uteuzi wa vipengele vya lugha katika tamthiliya teule unafanana au kutofautiana vyi katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii?
- (iii) Ni dhamira zipi zinajitokeza katika tamthiliya teule?
- (iv) Uteuzi wa dhamira katika tamthiliya teule unafanana au kutofautiana vyi katika kufikisha ujumbe kwa jamii?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti ni sayansi ya uchunguzi ambao ni muhimu kwa jamii. Katika uchunguzi wa matumizi ya lugha katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyrere na Safari ya Kanaani* utafiti umesaidia kuelimisha jamii kuona jinsi gani hawa wapigania haki Nyerere na Kinjeketile walivyokuwa wazalendo na dhamira ya ukombozi katika nchi yao. Utafiti pia umeonesha jinsi Nyerere na Kinjeketile walivyohamasisha watu wao kupigania uhuru wao. Kukataa kutawaliwa na kuonewa pasipo na sababu za msingi. Pia umegundua jinsi wananchi walivyokuwa na umoja katika kupigania uhuru waohadi kujikombua na kujitoa katika makucha ya wakoloni.

Aidha utafiti huu utakuwa changamoto kwa watafiti wengine kufanya utafiti juu ya tamthiliya za Kiswahili zilizojikita katika historia ya mambo mbalimbali yaliyotokea katika jamii.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umetathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*.

Zipo tamthiliya nyingi za kihistoria lakini kwa sasa nimeshughulikia tamthiliya za kihistoria za *Kinjeketile* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein na *Nyerere na Safari ya Kanaani* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Vipengele vya lugha tamathali za semi, misemo, methali na nahau ndivyo vimetumika katika kujenga hii kazi ya fasihi.

1.8 Uzingativu wa Maadili

Katika utafiti huu kipengele hiki cha uzingativu wa maadili umejadili masuala yaliyomwezesha mtafiti kuzingatia, na kudumisha maadili yake kabla na baada ya

kukusanya data. Masuala ya kimaadili huibuka katika aina zote za utafiti usio wa kitakwimu na ulio wa kitakwimu, Padget (2002) katika kipengele hiki mtafiti ametakiwa kuzingatia usiri, uwazi, utii, ushiriki wa hiari au kujitolea kwa watafitiwa bila kulazimishwa, kutokuwa na lugha chafu au kali, uvunjivu wa amani, na kuomba ruhusa ya utafiti wake katika maeneo aliyoyafanyia utafiti.

Aidha mtafiti wa utafiti huu aliomba kibali kilichomtambulisha kuwa yeye ni mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania cha kuingia katika maktaba ili kuweza kusoma tafiti za Kiswahili na machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu.

1.9 Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vya utafiti ni jumla ya changamoto mbalimbali zilizokabili utafiti huu. Changamoto hizo ni uhaba wa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti huu. Pia mtafiti ni mwajiriwa wakati huo huo anasoma hivyo amekabiliwa na changamoto ya muda wa kutafuta marejeleo, vitabu vya tamthiliya teule na kukutana msimamizi kwa maelekezo.

1.10 Utatuzi wa Vikwazo

Mtafiti alijiwekea mikakati mizuri ya kukabiliana na changamoto hizo ili aweze kufikia malengo ya utafiti wake. Ilibibidi mtafiti kubana matumizi kulingana ufinyu wa bajeti kutokana na pesa kidogo ya kugharamia utafiti huu. Pesa ilitoka kwa mtafiti mwenyewe na siyo kwa mfadhili. Hapa mtafiti ilimbidi kutumia pesa aliyoandaa kwa usahihi. Mtafiti aliangalie safari zake kwa umakini ili kuepuka gharama zisizo za lazima. Aidha kuhusu suala la muda, mtafiti alifanya shughuli hizi

jioni baada ya kazi na wakati mwingine ilimlazimu kuomba ruhusa ili aweze kuonana na msimamizi kwa maelekezo juu ya utafiti wake.

1.11 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu umegawanyika katika sehemu tano. Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti, uchunguzi umeonesha kuwa tatizo la utafitilimejadiliwa na kutolewa maelezo kwa undani. Sura ya pili inahusu usomaji wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, ambapo sura ya tatu imejadili mbinu za utafiti, mbinu za ukusanyaji data, na zana za utafiti. Sura ya nne imeonesha uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Aidha sura ya tano imewasilisha muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya mtafiti.

1.12 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, uzingativu wa maadili vikwazo vya utafiti, utatuzi wa vikwazo na muundo wa tasnifu. Sura inayofuata inawasilishamapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii maandiko na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti zimejadiliwa kwa kina na mwisho kuibua pengo la utafiti ambalo limeweka msukumo wa kufanya utafiti huu. Sura hii imeelezea dhana ya fasihi linganishi. Sehemu ya pili inahusu tafiti kuhusu tamthiliya za Kiswahili. Aidha sura hii imefafanua, pengo la utafiti, matumizi ya lugha, kiunzi cha nadharia, na hitimisho.

2.2 Dhana ya Fasihi Linganishi

Jilala (2016) akiwanukuu Wallek na Warren (1948), anasema fasihi linganishi ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kwa kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Ulinganishi unaweza kuwa wa fasihi ya Kiafrika na kizungu, ama fasihi ya kizungu dhidi ya Kihindu n.k. Guyard (1964) anasema kuwa fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi ambapo anadai ni somo la mahusiano, mapatano na maelewano ya kimataifa baina ya kazi na maisha ya waandishi wanaotoka katika fasihi tofauti.

Jilala (2016) akimnukuu Wamitila (2003), ameizungumzia dhana ya fasihi linganishi kwa kusema kuwa ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kueleza sifa mfanano zilizopo katika matini ya fasihi. Na kwamba dhana yenye huenda sambamba na dhana ya ulinganuzi. Ulinganuzi ni mbinu ya kuchunguza, kuchambua na kuonesha sifa zinazotofautiana baina ya matini zaidi ya moja za kifasihi. Kwa hiyo ulinganishi

na ulinganuzi sharti uzingatie fani na maudhui. Fasihi ya Wamitila inatupatia jambo jipya kuzingatia upamoja wa dhana za kulinganisha na kulinganua.

Kwa upande mwingine Van Tieghem kama alivyonukuliwa na Wallek (1988) anafasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili. Vitu hivi vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi wa kundi la waandishi au kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wake Wallek (1988) anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo la fasihi nnje ya mipaka ya nchi moja ni kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo jingine la maarifa, sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi na dini. Kwa upande mwingine anaielezea kwa ufupi kuwa ni ulinganishi wa fasihi na fasihi nyininge na ulinganishi wa fasihi mzunguko wa maelezo ya binadamu.

Ponera (2014) anasema fasihi linganishi ni kitendo cha kulinganisha au kufanya tathmini ya vitu viwili au zaidi ili kujua ubora, kufanana au kutofautiana kwavyo. Mtu yejote anayehitaji kulinganisha au kufanya linganisho lazima atahitaji kwanza kuwa na mahitaji kwa ajili ya kazi hiyo. Mosi, anhitaji kuwa na maarifa na ujuzi juu ya vilinganiswavyo. Pili, kuwapo kwa vitu viwili au zaidi vinavyolinganishwa. Na tatu, kuwapo kwa kigezo au vigezo maalum vyta kulinganishia.

Bassnett (1993) anaiona fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tofauti ili kubaini mazingira yanapokutana na yanapoachana. Nao Wallek ona Warren (1996) wanaielezea fasihi linganishi kuwa ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi, hata wanaulimbe kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni.

Fasihi linganishi hujihusisha na ulinganishaji wa fasihi na kazi nyingine ambazo ni za kisanii, kwa mfano mlinganishi anaweza kuchunguza uhusiano wa filamu na fasihi, kazi za sanaa ya uchongaji, uchoraji na uhunzi na fasihi. Aidha, kwa kutumia fasihi linganishi, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za mwandishi mmoja katika vipindi tofauti ama katika kipindi kimoja cha kihistoria. Kwa mfano tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za Shaaban Robert katika vipindi tofauti vyta uandishi au kulinganisha kazi za fasihi za Semzaba za kipindi cha miaka ya sabini na kipindi cha miaka ya elfu mbili. Hii itatuonesha kufanana, kutofautiana na kuhusiana kwa uteuzi na matumizi ya lugha na maudhui yanayowasilishwa na namna yanavyowasilishwa.

Pia katika fasihi linganishi, tunaweza kulinganisha kazi za fasihi za wasanii wanaotoka katika maeneo tofauti ya kijiografia, au eneo moja la kijiografia au wenge utamaduni mmoja. Kwa kufanya hivyo tunaweza kuibua matumizi ya lugha na vipengele vyake na dhamira zinazojitokeza ambazo zinawafananisha au kuwatofautisha wasanii. Tunaweza kusema kuwa fasihi linganishi ni mbinu inayohusisha ulinganishaji wa kazi za fasihi kwa lengo la kuchunguza jinsi kazi hizo zinavyofanana, na kutofautiana katika matumizi ya lugha na vipengele vyake na dhamira zinazojitokeza. Hivyo utafiti huu ni utafiti linganishi unaolenga kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya za *Kinjeketile* (1969) na *Nyerere* na *Safari yaKanaan* (2015). Lengo la utafiti huu ni kubainisha vipengele vyta lugha na dhamira pia kuona jinsi vinavyofanana na kutofautiana.

2.3 Tafiti kuhusu Tamthiliya za Kiswahili

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu tamthiliya za Kiswahili lakini nyingi zilijikita katika kuchambua lugha na maudhui kwa ujumla na si kutathmini matumizi ya lugha

na dhamira ambazo zimetumika katika utafiti huu. Kazi hizo ni za Kinge'i (1987), Ligembe (1995), Ramadhani (2005), Saleem (2013) na Mkuhwili (2014).

Kinge'i (1987) utafiti wake ulikuwa juu ya tamthiliya za msanii Ebrahim Hussein. Katika utafiti wake Kinge'i alimtaja Hussein kuwa ni mionganini mwa watunzi maarufu wa tamthiliya za Kiswahili. Tamthiliya za Hussein amabazo Kinge'i amezichambua ni *Alikiona* (1970), *Wakati Ukuta* (1970) na *Arusi* (1980) na kuona kuwa msanii huyu ana uwezo mkubwa wa kutumia lugha kama chombo cha kusafirishia ujumbe au maudhui yake katika jamii. Katika nadharia tumeona kuwa lugha ndiyo inayobeba kazi yote ya fasihi kutegemeana na jinsi lugha hiyo ilivyotumika. Utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Kinge'i kwa kuwa utafiti huu ni linganishi unaolinganisha kazi mbili za wasanii tofauti waliobobeaa katika ya uandishi wa fasihi zaidi ya miongo mitatu. Katika tamthiliya zao tumetumia tamthiliya moja ya hivi karibuni ya Mbogo (2015) *Nyerere na Safari ya Kanaani* na tamthiliya ya ilioandikwa zamani Hussein (1969) *Kinjeketile* katika kutathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika kufikisha ujumbe kwa jamii.

Ligembe (1995) alichambua sitiari katika kazi ya tamthiliya ya Lina Ubani iliyoandikwa na Penina Mhando. Katika utafiti wake amejadili muundo na umbo la tamthiliya na kubainisha aina za sitiari. Amebainisha kiungo kifananishi na kizungumzwa na kuelezea mchango wake katika uelewa wa tamthiliya. Katika utafiti wake hakuonesha uhusiano uliopo baina ya aina ya sitiari na ujenzi wa maana katika tamthiliya. Tofauti na utafiti wa Ligembe, utafiti huu ni utafiti linganishi ambao ulilenga kulinganisha na kulinganua kazi za tamthiliya za waandishi wawili ili

kubaini vipengele vya lugha vinavyowafananisha na kuwatofautisha katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Ramadhan (2005) alifanya utafiti kuangalia matumizi ya sitiari katika tamthiliya ya *Morani* iliyoandikwa na Mbogo na *Mashetani* iliyoandikwa na Hussein. Alitumia utafiti linganishi kwa kutumia nadharia ya elimumtindo ambapo amelinganisha tamthiliya mbili. Alihitimisha kuwa sitiari hutumika katka ujenzi wa dhamira mbalimbali katika tamthiliya zote mbili. Tofauti na utafiti alioufanya Ramadhan utafiti huu ulijikita katika kutathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule, kwa kutumia nadharia ya fasihi ya jamii kwa kuwa inahifadhi historia ya jamii.

Saleem (2013) alifanya utafiti linganishi katika wa tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Katika tasnifu yake ya uzamivu alibaini tamthiliya ya *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* zinafanana na kuhusiana katika mbinu za kimtindo na maudhui yake. Tofauti na utafiti wa Saleem, utafiti huu ulihusisha kutathmini vipengele vya lugha na dhamira zilijitokeza katika tamthiliya teule kwa kulinganisha na kulinganua vipengele hivyo.

Mkuhwili (2014) alifanya utafiti linganishi katika tamthiliya za *Ngoma ya Ngw'anamalundi* na *Kivuli kinaishi*. Lengo lilikuwa ni kulinganisha katika tamthiliya hizo. Alibaini kuwa wasanii hawa wanatofautina na kufanana katika baadhi ya vipengele vya kifani. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya elimumtindo ambao unamtofautisha msanii mmoja na mwigine katika mtindo wa uandishi wa

kazi ya fasihi. Tofauti na utafiti wa Mkuhwili, utafiti huu umetathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

2.4 Pengo la Utafiti

Tafiti zimekwishafanywa juu ya ulinganifu wa kazi za tamthiliya. Utafiti haukutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika fasihi linganishi kwa kuwasilisha jambo la kihistoria. Utafiti huu unahitajika ili kuweza kutathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya tofauti na waandishi tofauti. Utafiti huu ili ufikie lengo umetathmini matumizi ya lugha na dhamira zilizojitokeza katika kuwasilisha ujumbe, mtafiti ametumia tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*.

2.5 Matumizi ya Lugha

Jilala (2016) anasema lugha ni kipengele muhimu katika kazi za fasihi kwani ndiyo daraja linalounganisha hadhira na msanii katika mawasiliano. Katika kazi ya fasihi lugha hubeba dhamira, migogoro na ujumbe mbalimbali aliokusudia mtunzi kwa kazi hiyo ya fasihi. Ni kipengele muhimu sana kwa sababu hutofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji na uchongaji. Tunapojadili matumizi ya lugha katika kazi za fasihi tunazingatia vipengele vifuatavyo: misemo, nahau, methali tamathali za semi na lugha za wahusika, hasa lahaja zao (Senkoro, 2011). Sehemu inayofuata inajadili vipengele vya lugha

2.5.1 Tamathali za semi

Jilala (2016) tamathali za semi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wakati wanapofanya kazi ya fasihi ili kutia nguvu katika maana na hata sauti katika

maandishi ama maneno. Wakati mwingine tamathali za semi hutumiwa kwa njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu katika lugha. Ni semi zenyе kupanua, kupuuza au kubadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa na mtunzi kwenda kwa hadhira.

Wamitila (2003) anasema tamathali ya (za) semi hutumika kuelezea fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Kwa ujumla tunaweza kusema tamathali za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa kutumia dhana nyingine tofauti au zinazofanana nazo ambazo hutumiwa kwa lengo la kupanua, kupuuza, kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida, ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwahadhira au jamii mahsus.

Senkoro (2012) anaainisha tamathali za semi kuwa ni sitiari, tashibiha, metonomia, tashihisi, majazi, ishara, taashira na kejeli. Tamathali za semi huweza kutumika katika ulinganishi wa kazi za fasihi kwa kulinganisha na kulinganua jinsi zillivyotumika katika kazi moja na nyingine. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kuwa tamathali zinazotumika zaidi katika ushairi ni tashibiha, tashihisi, kejeli, metonimia, na sitiari.

Na tamathali zinazotumika zaidi katika kazi za kifasihi hasa katika tamthiliya na riwaya ni tashibiha, takriri, tanakalisauti, nidaa, sitiari, kejeli, tashihisi, tafsida, tashtiti na mdokezo. Katika sehemu hii mtafiti ameeleza maana ya tamathali chache zitakazotumika katika utafiti huu, ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Sehemu ifuatayo inajadili kuhusu tamathali za semi.

2.5.2 Kejeli

Hii ni tamathali ambayo maneno yake huwa kinyume kabisa na maana inayokusudiwa mfano mtu ni mchafu hukuna mfano wake lakini anaambiwa ye ye ndiye msafi kuliko wote. Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981:105) wanasema kuwa kejeli ni maneno ya dharau, fanyia mzaha wa kuchosha.

Kamusi ya Wales (2001:224) inasema, kuwa kejeli hutokea pale ambapo maneno yanayotumiwa yanaelekea kukinzana na maana inayohitajika katika muktadha maalum inayokusudiwa na mwandishi, msemaji au mtumiaji. Huangalia mbinu ya ulaghai, kinyume cha mambo, udanganyifu au masimulizi yasiyo ya kweli ndani yake katika kuzungumzia kumkebehi au kumteta mtu fulani.

Short (1980:277) anafafanua kuwa mbinu ya kejeli ni ushirikiano kati ya mwandishi au msemaji na msomaji au msikilizaji au hadhira. Mbatiah(2001) anasema kuwa kejeli ni maneno yanayotumiwa katika matamshi kwamadhumuni ya kuchoma, kukata, au kutia uchungu.Wamitila (2008:410) anaendelea kusema kuwa kejeli ya kiusemi inaelezwa kama ni kejeli ya kimsingi sana na hutokea pale ambapo pana mkinzano fulani baina ya kile kinachosemwa na uhalisia wenyewe.

2.5.3 Sitiari

Jilala (2016) anafafanua sitiari ni tamathali ya semi inayoltinganisha vitu viwili bila vilinganishi vyovyote. Ni ulinganishi wa moja kwa moja mfano Bwana Juma ni simba. Muundo wa sitiari una vipengele vitatu yaani kile knachozungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff na Johnson 1980). Ili kuelewa dhana ya sitiari tutumie mfano huu Juma ni simba. Katika mfano huu Juma amegeuka kuwa simba yaani

mnyama; bali sifa za simba zinahamishiwa kwake. Yaani simba ana sifa ya ukali unaosababishwa na simba anahusishwa na ukali wa Juma. Muundo wa sitiari una vipegele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff & Johnson, 1980; Kahigi 1995). kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu ni Juma; Kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano wetu ni simba na kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni sifa ya ukali.

2.5.4 Tashihisi

Katika tamathali hii vitu visivyo na sifa walizonazo binadamu hupewa sifa hizo mfano baridi kali ilimkaribisha alipofika Makambako. Wamitila (2003) anasema tashihisi ni tamathali ya semi vitu visivyokuwa na uhai huwasilishwa kwa namna sawa na binadamu na kuweza kufikiri na kuhisi sawa na afanyayo binadamu.

2.5.5 Tashibiha

Senkoro (1982) anafaili tashibiha ni tamathali ya semi ambayo watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa kwa kutumia vilinganishi kama vile mithili ya, mfano wa, kama, sawa na, kama kwamba mfano Juma ni mweusi kama mkaa. Hapa tashibiha imetumika kulinganisha rangi ya bwana Juma na mkaa. Dhana hii ya ulinganishaji hutumika tabia, sifa zinazolininganishwa hivyo weusi wa bwana Juma unalinganishwa na mkaa.

2.5.6 Takriri

Ni mbinu ya kurudiarudia maneno kwa ajili ya kusisitiza jambo, mfano kwenye nyimbo na mashairi, tamathali hii hutumika zaidi. Jilala (2016), akiwanukuu Kahigi

na Mulokozi (1979), anaielezea takriri kuwa ni uradidi yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi na hata sentensi katika kazi za kifasihi.

2.5.7 Nidaa

Huu ni msemo ambao unaonesha kushangazwa kwa jambo fulani na kuambatana na matumizi ya alama ya mshangao, mfano Lo! Kumbe! La hasha!.Senkoro (2011) anasema kuwa nidaa ni msemo uanoonesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani, mfano Haa! Hicho ni kifurushi cha mafumbo!.

2.5.8 Tashtiti

Tashtiti ni mkazo wa maneno yasemayo au kuandikwa. Msanii hutumia mbinuya kuuliza maswali kwa jambo ambalo analolifahamu jibu lake. Lengo ni kusisitiza jambo na kuleta mshangao (Msokile 1992:62).

2.5.9 Mdokezo

Mdokezo ni tamathali ambayo mtu hudokeza kitu fulani na kukiacha bilakukikamilisha kwa maana kwamba kinaweza kukamilishwa na mtu mwingine kisanaa. (J.P.OCompany2008:45). Jilala (2016) akiwanukuu Cuddon (1998), anafasili kuwa mdokezo ni mbinu ya msanii kuishirikisha hadhira yake uzoefu fulani wa maisha.

Mara nyingi msanii wa kazi ya fasihiatumiaipo mdokezo katika kazi ya fasihi anakuwa na lengo la kumfikirishamsomaji au hadhira juu ya jambo analolizungumza. Hivyo ni jukumu la hadhira kufikiri na kukamlisha wazo la msanii katika kazi yake kifasihi.

2.6 Dhana ya Dhamira

Kwa mujibu wa Jilala (2016), anasema dhamira ni jumla ya mambo yanayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Senkoro (1982) anasema dhamira za kazi za fasihi hujitokeza kulingana na matukio ya jamii, wakati, mabadiliko ya jamii na historia ya jamii. Kwa mfano dhamira zilizoibuliwa kipindi cha ukoloni zililenga kuibua suala la ukoloni na unyonyaji.

Senyamanza (2012) anaeleza kuwa dhana ya dhamira isichanganywe na dhana ya maudhui kwa sababu dhana hizo ni tofauti. Hivyo aliwanukuu TUMI (1992), kuwa dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi katika kazi yake. Dhamira ni sehemu mojawapo tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Kwa ujumla dhamira kuu ndiyo husindikizwa na dhamira ndogo ndogo na hizi ndizo zijengazo dhamira kuu. Wazo kuu ambalo hasa ndilo libebalo wazo kuu hutoa dhamira kuu.

Naye Madumula (2009) anaunga mkono mawazo ya TUMI, akielezea kuwa dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Anaendelea kuelezea kuwa Senkoro anatahadharisha kuchanganya dhamira na maudhui jambo ambalo hutokea kwa wengi. Dhamira ni sehemu tu ya maudhui. Na aghalabu dhamira kuu ndio husindikizwa na dhamira ndogondogo. Wazo kuu hubeba funzo kuu.

Kwa mujibu wa Jilala (2016), katika kipindi cha janga la UKIMWI duniani, wasanii walielekeza jicho la kisanii katika kuibua dhamira zenye lengo la kuonesha matatizo, chanzo, dalili, uenezaji na namna ya kujikinga na athari ya UKIMWI katika jamii. Dhamira ni kipengele ambacho kinaweza kuhusishwa katika ulinganishaji wa kazi za fasihi. Dhamira hutusaidia kuonesha wasanii wanavyotofautiana katika kuibua

matukio ya kijamii na kuimulika jamii kwa tochi ya kisanii. Kwa kulinganisha dhamira za kazi mbalimbali za fasihi tunaweza kubaini muingiliano na mahusiano ya dhamira za duniani, kuhama kwa dhamira na kusambaa kwa dhamira kulingana na wakati, mazingira na muktadha.

2.7 Kiunzi cha Nadharia

Jilala (2016) anasema nadharia ni wazo ambalo huibuliwa kama mwongozo kwa msomaji ama mchambuzi na hata mwanafasihi linganishi katika kutoa majumuisho ya kazi za fasihi. Aidha ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo wa mtu au watu jamii ya mahali fulani wakati fulani kwa lengo maalum. Nadharia humwongoza mtu kutenda jambo fulani kwa utaratibu mzuri. Kwa hiyo nadharia ndiyo msingi mkuu wa kuweza kueleza jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika ama taaluma ya fani husika.

Wanjala (2011) anasema nadharia ni mwongozo au maarifa yanayotumiwa na binadamu kwa kukabiliana na mazingira yake. Au nadharia ni mfumo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsus kwa kutoa mtazamo au falsafa juu ya matumizi na taratibu za utafiti.

Sengo (2009) anasema nadharia ni wazo kuu, fikra, mwongozo mkuu wa mtu au watu (jamii), wa pahala fulani wakati fulani kwa sababu fulani. Kuna nadharia za aina mbalimbali zinazotumika katika kuchunguza na kuchambua kazi mbalimbali za fasihi. Nadharia fulani inaweza kufaa kutumika kuchambua kazi ya fasihi na nadharia nyingine isiweze kufaa kutumika kuchambua kazi hiyohiyo kulingana na

malengo ya utafiti huo. Baadhi ya nadharia zinazoweza kuchambua kazi za fasihi ni ufeministi, umuundoleo, umaksi, elimumtindo, nadharia ya fasihi ya jamii na mwitkio wa msomaji. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya fashi ya jamii.

2.7.1 Nadharia ya fasihi ya jamii

Uhusiano wa fasihi na jamii umethibitishwa kupitia fasili nyingi za fasihi na uhusiano wa taasisi hizi mbili hauwezi kupuuzwa hivyo fasihi ni taasisi ya jamii. Mmoja wa wanaounga mkono dhanna hii ni Escarpit (1974), ambaye anasema, fasihi ni lazima ichukuliwe kama iliyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii. Fasihi ni taasisi ya jamii kwani hutumia lugha ambayo ni wazo la jamii kwamba fasihi ni sehemu ya maisha ya jamii. Maisha kuhusu uhalisiya wa jamii, hata kwa mtu binafsi ni mambo ambayo fasihi inazingatia. Kwa hiyo fasihi inayo dhima kuu katika jamii. Nao Wallek na Warren (1949), wanashadidia kwa kusema, “Uhusiano kati ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kuanza na kauli aliyoitoa De Bonaid kwamba “Fasihi ni kielelezo cha jamii.” Kwa kutumia nadharia ya fasihi ya jamii tumeona kuwa utafiti huu uliweza kuonesha vipengele vya lugha vilivyotumika na dhamira zilizojitokeza na pia kufananana na kutofautiana kwake.

Kwa kupitia nadharia hii, moja ya kazi za fasihi ni kuhifadhi historia ya jamii hiyo. Mfano, vipindi maalum vya mfumo wa maisha ya jamii. *Morani* (Mbogo 1993) na *Kivuli Kinaishi* (Mohamed 1990) ni mfumo wa unyonyaji. Unyanyasaji, rushwa na uongozi mbaya kwa jamii ya Tanzania. Zote hizo ni mifumo ya jamii katika Nyanja za maisha pamoja na matumizi ya lugha na vipengele vyake. Hivyo basi mtafiti anaona kwamba kauli ya fasihi ina uhusiano mkubwa na jamii ni dhima yenye mashiko. Tunasema ni muhimu kuichukulia fasihi kama zao la jamii ambalo

nalohathiri na kuathiriwa na jamii hiyo. Nadharia hii pia inatoa mchango kwa kuonesha historia ya jamii hiyo matukio mbalimbali yaliyotokea na jinsi jamii ilivyojifunza, ilivypambana na mafanikio yaliyopatikana.

2.8 Hitimisho

Katika utafiti, sura hii ni ya muhimu sana kwa kuwa imeonesha katika kazi za kifasihi jinsi watafiti wengine walivyofanya utafiti. Na katika kazi hizo mtafiti alichagua baadhi ya kazi zinazohusiana na utafiti huu. Kupitia kazi tangulizi mtafiti aliweza kugundua watafiti wengine walifanya nini na jinsi walivyochambua data, tatizo la utafiti lilikuwa nini, pengo la utafiti na maarifa yaliyoweza kutumika katika kazi ya fasihi. Sura hii imeanza na kazi tangulizi kwa kuchunguza dhana ya fasihi linganishi. Kupitia wataalamu mbalimbali kwa mawazo yao. Vilevile mtafiti amepitia tamthiliya za Kiswahili ambapo aliweza kuona tafiti nyingi zilichunguza fani na maudhui. Kupitia tafiti hizo imebainika kuwa tafiti linganishi katika lugha na vipengele vya vyake na dhamira katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani* hazijafanyika, hivyo kumfanya mtafiti awe na ari ya kufanya utafiti huu. Pengo la utafiti limeonekana wazi ambalo ndilo limewezesha utafiti huu kufanyika.

Pia sura hii imeangalia kiunzi cha nadharia ya fasihi ya jamii ambayo ndiyo imetumika kuchunguza matumizi ya lugha na vipengele vyake na dhamira katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Sura inayofuata inawasilisha mbinu na njia za utafiti.

SURA YA TATU
MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imejadili mkabala wa utafiti, mbinu na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya na kuzichambua data zilizopatikana. Utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana (Kombo na Tromp, 2006) (Opie, 2004) anasema mbinu na njia zina maana ya mikakati inayowekwa katika kukusanya na kuchambua taarifa kwa kupata ukweli, ili kusuluuhisha jambo, kujibu swalii au kutatua tatizo. Hivyo mbinu ni mpangilio maalum wa mikakati anayoiandaa mtu kwa ajili ya kufanikisha jambo fulani kwa urahisi. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu na njia tofauti ambazo zilimwezesha kupata data za matokeo sahihi na zenye ubora wa kufikia mwisho mwema. Miongoni mwa mbinu hizo ni usomaji matini mbalimbali zilizohusiana na utafiti huu.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eno la jiji la Dar es Salaam ambapo utafiti ulifanyika kwa kusoma katika maktaba mbalimbali kama vile Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na Maktaba Kuu Tanzania.

3.3 Kundu Lengwa

Kulingana na Kothari na Brayyman (2004), Kombo na Tromp (2006) wanasema kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Katika utafiti

huu kundi lengwa ni tamthiliya za *Kinjeketile* iliyotungwa na msanii E.Hussein na Nyerere na *Safari ya Kanaani* iliyotungwa na msanii E. Mbogo.

3.4 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kouchaguloiowa kupoata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Katika utafiti huu mtafiti ametumia usampulishaji lengwa. Hio ni aina ya sampuli ambay watafitiwa ama vitafitiwa ambavyo mtafiti amejiridhisha kwamba watafitiwa hao watampatia data zitakazomwezwsha kutimiza malengo ya utafiti wake (Yin, 1994). Aina hii ya usampulishaji imetumika katika kuteua tamthiliyoa za *Kinjeketile* na Nyerere na *Safari ya Kanaani*.

3.5 Sampuli

Sampulini istilahi inayotumika kumaanisha watu walioteuliwa kujibu maswali ya utafiti katika kundi husika (Kothari, 1990). Hivyo katika utafiti sampuli ilikuwa ni vipengele vya lugha na dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

3.6 Mbinu za ukusanyaji data

Katika utafiti mbinu mbalimbali huweza kutumika katika kukusanya data, kama Scale (2012) na Silvaman (2010) wanavyounga mkono hoja wanassema kuwa kuna mbinu mbalimbali za kukusanya data lakini si kila mbinu inafaa kwa kila utafiti. Mbinu itakayotumika itategemea na mazingira, wakati na aina ya utafiti. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya maktaba na usomaji matini mbalimbali.

3.6.1 Mbinu ya Usomaji Matini Mbalimbali

Maktaba ni mkusanyiko wa vitabu vilivyohifadhiwa kwa ajili ya kusoma, TUKI (2004). Mtafiti alitumia njia ya usomaji taarifa mbalimbali zinazohusiana na utafiti

huu ambazo zimekwishaandikwa vitabuni, magazetini na kwenye majarida na kazi za tafiti zilizohusu tamthiliya za kiswahili. Vitu vingi hupatikana katika maktaba ambavyo mtafiti alitarajia kuvitumia, kulingana na malengo ya utafiti wake.

Mbinu hii ilitumika katika utafiti huu ambapo mtafiti alisoma na kuchambua vitabu vya *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani*, pamoja na vitabu vingine vya ziada ili kumwezesha mtafiti kupata data muhimu katika utafiti huu, na kukidhi mahitaji ya utafiti uliolengwa. Kwa kusoma vitabu vitakavyopatikana katika maktaba mtafiti aliweza kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya hizo ambapo ilimwezesha kugundua namna vipengele vya lugha vinavyofanana au kutofautiana na jinsi lugha ilivyotumiwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

3.7 Zana za Utafiti

Mulokozi (1983) anaeleza kuwa zana za utafiti ni vifaa vya utafiti hutegemea aina ya utafiti. Aghalabu baadhi ya vifaa hivi kama si vyote hutumika, kalamu, karatasi, shajala ya uwandani, tepu rekoda na vifaa vyake, kamera na vifaa vyake, kompyuta, daroubini, vifaa vya kupimia, kuhesabu, matini, nakadhalika.

Zana za utafiti ni muhimu sana kwa mtafiti ambazo ni kalamu na karatasi kwa ajili ya kuandika na kutunzia kumbukmbu muhimu zitakazopatikana wakati wa kusoma katika maktaba(Kabuk 1987). Zipo zana za aina mbalimbali za utafiti, ilamtafiti katika utafiti huu alitumia baadhi ya hizo ambazo zimefafanuliwa hapa chioni:

3.7.1 Matini

Hivi ni vitabu vilivyotumika katika utafiti huu kwa ajili ya kutathmini matumizi ya lugha na dhmira ambavyo ni *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari ya Kanaani* pamoja

na vitabu vingine nya kiuhakiki ambapo matini hizi zilitoa mchango katika utafiti huu kwani data za matumizi ya lugha na dhamira zilipatikana na kuufanya utafiti ufikie lengo la kuwasilisha ujumbe kwa jamii au hadhira iliyokusudiwa.

3.7.2 Kompyuta

Kompyuta ilitumika katika kutafutia matini kutoka katika tovuti na wavuti, na pia kuhifadhi taarifa mbalimbali zilizohusiana na utafiti huu. Data zilizohifadhiwa hutolewa mahitimisho.

3.7.3 Simu ya mkononi

Mtafiti alitumia simu ya mkononi ambayo ilimsaidia na kumrahisishia kupata mawasiliano na msimamizi kwa ajili ya kupata maelekezo na jinsi yakuwasiliana naye na kufanya masahihisho.

3.8 Hitimisho

Sura hii imejadili mbinu na njia za utafiti ambapo eneo la utafiti limebainishwa , kundi lengwa, mbinu ya ukusanyaji data, na zana za utafiti. Katika ukusanyaji wa data mtafiti alitumia mbinu ya maktaba kwa kusoma vitabu na machapisho mbalimbali ya kazi za fasihi. Aidha mtafiti alionesha umuhimu wa zana za utafiti na jinsi zilivyotegemeana na kuweza kufanikisha utafiti huu. Sura inayofuata inawasilisha uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu nne. Kipengele cha kwanza kinazungumzia lugha na vipengele vyake katika tamthiliya teule. Kipengele cha pili inazungumzia damira zilizojitokeza katika tamthiliya teule. Tatu kulinganisha na kulinganua vipengele ya lugha. Mtafiti ameendelea kulinganisha na kulinganua dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *safari ya Kanaani*. Na kipengele cha mwisho ni hitimisho.

4.2 Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya Teule

Kati ya malengo mahsusini ya utafiti huu ni kulinganisha vipengele vya lughakatika tamthiliya teule. Vipengele hivyo ni methali, nahau, tamathali za semi na misemo. Vipengele vimechambuliwa kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mbinu ya usomaji wa machapisho imetumika ili kuweza kupata data na kuweza kuchambua tamthiliya teule. Pia mtafiti amepata data kuitia maandiko mbalimbali. Mtafiti amebainisha vipengele vya lugha viliviyotumika katika tamthiliya teule za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya kanaani*, baadhi yake ni kama ifuatavyo:

Jedwali Na 4.1: Vipengele vya lugha katika Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Kipengele cha lugha |
|-------|---------------------|
| 1. | Methali |
| 2. | Nahau |
| 3. | Tamathali za semi |
| 4. | Misemo |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanani* (2016)

Data za utafiti huu zimedhihirisha mwandishi huyu ametumia methali, nahau, tamathali za semi, na misemo katika utunzi wa kazi hii ya kifasihi. Vile vile mtafiti amechambua vipengele vya lugha katika tamthiliya ya *Kinjeketile*, katika Jedwali namba 4.2.

Jedwali Na 4.2: Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Kipengele cha lugha |
|-------|---------------------|
| 1 | Tamathali za semi |
| 2 | Methali |
| 3 | Misemo |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Data zinaonesha kuwa msanii huyu ametumia tamathali za semi na misemo katika utunzi wake wa kazi ya fasihi. Utafiti umegundua kuwa msanii Husseni ametumia vipengele vitatu vya lugha katika ujenzi wa kazi yake. Mtafiti wa utafiti huu amechunguza matumizi ya vipengele hivyo kwa lengo la kufanya utafiti linganishi katika tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na safari ya kanani*.

4.3 Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya za *Kinjeketile na Nyerere na Safari ya Kanaani*

Utafiti huu ulichunguza mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika tamthiliya teule za kihistoria kama ifuatavyo:

Jedwali Na 4.3: Mdafao wa Ujitokezaji wa Vipengele vya Lugha katika Tamthiliya ya *Kinjeketile na Nyerere na Safari yaKanaani*

| Namba | Kipengele cha lugha | Mdafao wa Ujitokezaji | |
|-------|---------------------|-----------------------|--------------------|
| | | <i>Nyerere</i> | <i>Kinjeketile</i> |
| 1 | Methali | 1% | 0.25% |
| 2 | Nahau | 1% | - |
| 3 | Tamathali | 96% | 97.75% |
| 4 | Misemo | 2% | 2% |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka *Nyerere na Safari yaKanani na Kinjeketile* (2016)

Jedwali namba 4.3 linawasilisha mdafao wa ujitokezaji wa vipengele vya lugha katika tamthiliya teule. Data zinadhihirisha kuwa msanii ametumia tamathali za semi katika *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* kwa asilimia tisini na sita (96) na asilimia zilizobaki ametumia katika vipengele vingine vya lugha. Pia data zinadhihirisha katika *Kinjeketile* tamathali za semi zimetumika kwa asilimia tisini na saba nukta saba tano (97.75) na misemo kwa asilimia mbili (2) na methali asilimia sifuri nukta mbili tano (0.25). Utafiti katika tamthiliya hizi za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanani* ulichunguza ujitokezaji wa vipengele kwa kila tamthiliya na jinsi zinavyotofautiana kwa kila moja ya tamathali hizo.

4.4 Uteuzi na Matumizi ya Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni usemi wenyewe kupanua, kupunguza, au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kishairi iliyokusudiwa na msanii au mtunzi (Kahigi na Mulokozi, 1979). Tamathali za semi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na sauti katika maandishi au kusema (Senkoro, 2011) tamathali hizi za semi ni kama ifuatavyo;

4.4.1 Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

Jedwali hapo juu linaonesha tamathali za semi zilizojoitokeza katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*. Utafiti huu ulichunguza ni kwa kiwango gani kila tamathali ya semi imetumika katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*. Mtafiti alitaka kujua tamathali ya semi iliyotumika mara nyingi zaidi katika kujenga kazi yake ya fasihi. Kwa kuchunguza matumizi ya lugha pia mtafiti amebaini

tamathali za semi zilizotumiwa na msanii katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Matokeo yameonesha kama ifuatavyo katika jedwali.

Jedwali Na 4.4: Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanani

| Namba | Tamathali za Semi |
|-------|-------------------|
| 1 | Tashihisi |
| 2 | Sitiari |
| 3 | Tashibiba |
| 4 | Tashititi |
| 5 | Takririri |
| 6 | Tanakali za sauti |
| 7 | Kejeli |
| 8 | Mdokezo |
| 9 | Nidaa |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani (2016)

Jedwali Na 4.5: Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanani

| Namba | Tamathali za semi | Mdafao wa ujitokezaji |
|-------|-------------------|-----------------------|
| 1 | Tashihisi | 15 |
| 2 | Sitiari | 17 |
| 3 | Tashibiba | 17 |
| 4 | Tashtiti | 7 |
| 5 | Takririri | 14 |
| 6 | Tanakali sauti | 1 |
| 7 | Kejeli | 3 |
| 8 | Nidaa | 234 |
| 9 | Mdokezo | 53 |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani (2016)

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa nidaa ni tamathali ambayo ilijitokeza kwa kiasi kikubwa zaidi ya tamathali nyingine kwa mdafao wa 234., ikifuatwa na mdokezo kwa mdafao wa 53, tashibiha na sitiari kwa mdafao wa 17. Tashihisi kwa mdafao wa 15. Takiriri nayo ilijitokeza kwa mdafao wa 14, tashtiti kwa kwa mdafao wa 7, tafsida kwa mdafao wa 6, ikifuatiawa na kejeli kwa mdafao wa 3 na mwisho tamathali iliyojitokeza kwa mdafao wa 1 ni tanakali sauti. Hii inadhihirisha kuwa msanii ametumia nidaa kwa kiwango kikubwa katika kujenga kazi yake ya kihishoria.

4.4.2 Nidaa

Mtafiti wa kazi hii alibaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari yaKanaani* ametumia nidaa kwa kiwango kikubwa na kuona kuwa nidaa ndioilyobeba ujumbe wa kazi hii. Msanii wa kazi hii, ametunga kazi hii ili kuonesha vijana wa Taifa kujenga uzalendo katika nchi yao. Vijana watambue kuangalia maslahi ya Taifa na kudumisha amani ya nchi. Kwa kujenga uzalendo huo vijanawamalizapo kidato cha sita au chuo kikuu walitakiwa kutumikia Jeshi la KujengaTaifa kwa mujibu wa sheria. Na wawapo katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa hujifunza mambo mbalimbali ya ujasiriamali na kazi nyingi za kujitegemea. Nidaa ni msemo ambao huonesha kushangaa na kushangazwa na jambo fulani. Misemo hii huambatana na alama ya kushangaa katika kukubali kuchukia au kuonesha heshima maalumu.(Msokile,1992:63) Nidaa ni msemo unaonesha kushangaa au kushangazwa na jambo fulani. Mfano Aa! Mbona unaondoka ghafla! Utafiti huu ulibaini baadhi ya nidaa katika tamthiliyahiiya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* kama ifuatavyo:

Jedwali Na 4.6: Mifano ya baadhi ya Nidaa katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Nidaa |
|-------|--|
| 1 | Siyo mchongameno! Anaitwa Hambiliki! |
| 2 | Aa! Mbona unaondoka ghafla! |
| 3 | Hapana! Nenda kwa Farida! |
| 4 | Anazo dawa kimbia mama nakufa! |
| 5 | Aa! Hufi, nakwambia! |
| 6 | Ukienda kumwita Farida haraka, sitakufa ---- Aaa! |
| 7 | Martini mwanangu, mwanamke!? |
| 8 | Niachie basi usiubofye mwili wangu, usije uknipasua mwenzio! |
| 9 | Aa! Watu wanatia chumvi tu! |
| 10 | Haiwezekani! Kwenda JKT miezi sita, kisha kukatwa 60% ya mshahara kwa miezi 18. Nani atakubali? |
| 11 | Mjinga we1 Babaako akitaka kukucharaza viboko, kwa utovu wa adabu, huwa anakupeleka kwa daktari kwanza?! Mimi nawacharaza nyote leo kama babaenu. Ninyi watoto wadogo?! Juzi tu mlikuwa mnavaa nepi na kutoka kamasi, ndiyo mnatutukana sisi, ninyi?! Lala chini Martin! |
| 12 | “We Zebedayo nini sasa! Tohara! Tohara! Kama wao wanapendana, wewe inakuhusu nini!” |
| 13 | Me, I am excited! Huu msamaha naukumbatia kwa mikono miwili |
| 14 | Mgonjwa! Mgonjwa! Mtoto laana tupu! Haya! Na ninyi ingieni ndani. Upesi! Nyama nyie! |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Tamthiliya ya Nyerere na *Safari ya Kanaani* (2016)

Msanii wa tamthiliya *Nyerere na Safari ya Kanaani* kutokana na data hizo hapo juu nidaa zilitumika kuwasilisha ujumbe wa kwa jamii au hadhira. Msanii alituonesha kuwa mwanamke anaweza, pale Martini alipomwambia mama yake akamwite Farida aje kumtibu. Mama yake alisita kwa kuona kuwa mwanamke hawezi, ni bora aende kumwita daktari aliystaafu ili kumtibu mwanaye. Mfano; “Hapana! Nenda kwa Farida anazo dawa. Kimbia mama nakufa! Aaa! Hufi nakwambia! Ukienda kumwita Farida haraka, sitakufa --- Aaa! Martini mwanangu mwanamke!?” Tunaona hadi leo hii bado mwanamke haaminiwi katika jamii kwa kiasi kikubwa. Hata katika

chaguzi mbalimbali mara nyingi wanawake wanaangushwa kwa kutokuaminiwa na jamii husika.

4.4.3 Tashibiha

Ni tamathali ya semi inayotumia sentensi kwa kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia vilinganishi, kwa mfano mithili ya, kama kwamba, sawa, kama vile, na kama. Mulokozi, (2002); Kahigi, (1995); Senkoro, (1982); wanasema tashibiha ni tamathali ya semi inayotoa mfano wa vitu unaojengwa kwa maneno kama vile kulinganisha vitu viwili au zaidi. Kwa kutumia vilinganishi kwa mfano mithili ya, kama vile, kama kwamba, sawa na mengineyo. Ujitokezaji wa baadhi ya tashibiha katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* uliochunguzwa na kubainishwa na utafiti huu umeoneshwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:

Jedwali Na 4.7: Tashibiha katika Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*

| Namba | Tashibiha |
|--------------|---|
| 1 | Amesimama imara kama mlima Kilimanjaro hatikisiki |
| 2 | Ndiyo katika nchi maskini kama hii mishahara yetu ni minono mno |
| 3 | Kurudi Misri kwangu mimi ni sawa na kumlazimisha mwislamu kula nguruwe |
| 4 | Macho haya yanayong'ara kama pacha ya nyota zinazowaka na kumeremeta juu ya mbingu samawati katika majira ya kiangazi |
| 5 | Hata akinikuta sebuleni ananipita tu kama hanijui. Ananiona kama shetani, kidudu kalikopotea njia |
| 6 | Rais gani duniani anaweza kuvumilia na kuyafumbia macho na masikio matusi na kebehi kama zile? |
| 7 | Tutawapata vijana majabari, wenye nguvu kama kifaru |
| 8 | Niko ngangari kama jabari la jibrota |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2016)

Msanii alitumia tashibiha katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* kuwasilisha ujumbe wa kazi hii ya fasihi kwa hadhira. Kwa mfano “Kurudi Misri kwangu ni sawa na kumlazimisha mwislamu kula guruwe. Ni kama kumlazimisha Mungu kumsamehe Lusifa.” Nyerere alimwambia Kambona haya maneno kwa kuonesha msimamo wake wa kuiteteta na kuijenga Tanzania ya Ujamaa wa kweli. Wananchi wanatakiwa kuwa wazalendo wa kuijenga nchi kwa uaminifu na kwa kushirikiana pamoja kwa nia moja. Wananchi wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii, juhudhi na maarifa kila mmoja kwa uwezo alionao ili kuinua uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Aidha mtunzi wa tamthiliya hii aliendelea kutumia tashibiha kama vile “Amesimama imara kama mlima Kilimanjaro.” Nyerere alikuwa na msimamo kuhusu vijana wamalizapo kidato cha sita na vyuo waende kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria, kwa lengo lakuwajengea uzalendowa nchi yao. Vijana hawa wakimaliza kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa waweze kujitegemea, kutetea nchi na wananchi wake kwa ujumla. Wawapo katika Jeshi la Kujenga Taifa wanafundishwa kufanya kazi mbalimbali, wanapewa mafunzo juu ya ulinzi wa nchi na hao ndio askari wetu wa akiba katika nchi yetu.

4.4.4 Tashihisi

Utafiti ulibaini kuwa msanii *wa Nyerere na Safari ya Kanaani* alitumia tashihisi kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa jamii. (Senkoro, 1982), anasema tashihisi ni tamathali ya semi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Kwa kuwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizo nazo binadamu hupewa sifa hizo.

Mfano “Kunguru hao walikuzomea wakisema, Babu jinga hiloooo!!!
Bwagedayooo!!! huyooo!”

Jedwali Na 4.8: Baadhi yaTashihisi Zilizojitokeza katika Tamthilia ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Tashihisi |
|-------|---|
| 1 | Akili zina breki kichwani; lakini hisia ni gurudumu, lenye wazimu halidhibitiki, bali huenda kasi na pengine hata kugonga mwamba. |
| 2 | Kunguru hao wakikuzomea, wakisema: “Babujinga hiloooo!!! Bwagedayooo!!! huyooo!” |
| 3 | Maguruwe pori toka ughaibuni yataletwa yaje kuuziwa rasilimali za nchi kwa bei chee. |
| 4 | Pengo kati ya nguruwe na walala hoi litakuwa bonde la ufa. |
| 5 | Kuwa kiongozi ni kuchagua utakatifu. Kukaa Ikulu ni kuchagua utakatifu. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka Katika Tamthiliya ya Nyerere na *Safari ya Kanaani* (2016)

Data katika jedwali namba 4.8 zinaonesha msanii alivyotumia tashihisi katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safariya Kanaani* ili kuwasilisha ujumbe katika jamii. Mfano “Maguruwe pori toka ughaibuni yataalikwa yaje kuuziwa rasilimali za nchi kwa bei chee.” Hapa msanii anamwonesha Nyerere alivyokuwa na uchungu na nchi ya Tanzania. Aidha aliwataka wanachi wasije wakaingiza watu wa nje kututawala ambapo tashihisi imewapa nguruwe sifa za binadamu. Msanii amewasilisha dhana ya uzalendo ambapo kila mwananchi wa Tanzania anatakiwa kuwa na uzalendo wa kujenga nchi, kuilinda dhidi ya maadui na kujenga umoja wa kweli.

4.4.5 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya semi inayotumika kuumba picha fulani inayoamsha mwetikio fulani kutoka katika hadhira . (Mulokozi, 2002). Utafiti huu ulibaini kuwa mtunzi

wa tamthiliya hii ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* ametumia sitiari, kwa kuwa sitiari ni tamathali inayohamisha maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. (Kahigi, 1995), anasema katika sitiari kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kuhusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine. Baadhi ya sitiari zilizojitokeza katika tamthiliya hii ni kama inavyoonekana katika Jadwali namba 4.9.

Jedwali Na 4.9: Sitiari katika Tamthiya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Sitiari |
|-------|---|
| 1 | Vyama vya upinzani vingekuwa kidhibiti-mwendo cha mseleleko wa kuelekea uimla wa chama tawala. |
| 2 | Kufutwa kwa vyama vya upinzani ni yai la mamba kisiasa. |
| 3 | Vitabu na maarifa ni chakula kisichoshibisha. |
| 4 | Tohara ni kama tupa na kinoo kinachoongeza makali ya mkuki na ufanisi vitani |
| 5 | Japokuwa wewe hukuwa chaguo la baba; lakini uchumba wetu haukulipua kombora la hasira ndani yake kiasi hichi. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2016)

Sitiari zilitumika katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Utafiti ulibaini kuwa msanii alizitumia sitiari ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Mfano “Vyama vya upinzani vingekuwa kidhibiti mwendo wa mseleleko wa kuelekea uimla wa chama tawala.” Hapa Kambona alimwambia Nyerere vyama vya upinzani viendelee kuwepo ili viweze kukisoa chama tawala. Pia aliendelea kumweleza Nyerere kwa kusema “Vyama vya upinzani ni dira ya kukuonesha makosa na uweze kujisahihisha pale unapofanya makosa ya kibinadamu au hata makosa ya makusudi.” Hivyo vyama

vingi vinaruhusu mtu kukosolewa anapoenda kinyume na matakwa ya wananchi ili wananchi hao waweze kupata haki zao.

4.4.6 Takriri

Takriri ni tamathali ya semi ambayo hurudiarudia sehemu ya neno au senntensi ili kuonesha msisitizo katika kila kinachozungumzwa au kinachoandikwa. Hivyo utafiti huu ulibaini mtunzi wa tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* alitumia baadhi ya takriri kama jedwali linavyoonesha.

Jedwali Na 4. 10: Ujitokezaji wa Takriri katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Takriri |
|--------------|--|
| 1 | Lakini “Musa! Musa!” Musa ni sawa. |
| 2 | Chwa! Chwa! |
| 3 | Sirudi! Sirudi! baba sirudi! Tukimbie! |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaan* (2016)

Takriri katika Jedwali namba 4.10 zilitumika na msanii kuonesha jinsi alivyoweza kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Mfano “Nitamcharaza mwanangu hapahaha mbele yako...” “Lala chini! Nasema lala chini Saigoda!” “Chwa! Chwa! ... Hapa mzee Mwajombe mzazi wa Saigoda alikasirishwa na kijana wake kuwa mtovu wa nidhamu kwa Rais Nyerere kwa kuungana na wenzake katika maandamano ya kupinga kwenda kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa. Mzazi huyu anaonesha ushirikiano wa yeye na serikali katika kumlea kijana wake. Mzazi huyu anaonesha kuwa tuwalee watoto kwa kuwajengea maadili ya kuwa na nidhamu. Vijana wawe na utii na

kuwaheshimu viongozi wanaowaongoza, endapo kuna haki wanayoidai basi wafuate utaratibu unaostahili ili kujenga uzalendo unaotakiwa.

4.4.7 Tashtiti

Katika tamthiliya hii ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* utafiti umebaini pia ujitokezaji wa tashtiti ambazo msanii alizitumia kuwasilisha suala la kihistoria katika jamii. (Msokile, 1992: 62),anasema tashtiti ni mkazo wa maneno yasemwayo au yaandikwayo. Msanii hutumia mbinu ya kuuliza maswali kwa jambo ambalo analifahamu jibu lake, kwa lengo la kusisitiza jambo na kuleta mshangao. Ujitokezaji wa baadhi ya tashtiti katika Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* kama Jedwali 4.11 linavyoonesha .

Jedwali Na 4.11: Ujitokezaji wa Tashtiti katika Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*

| Namba | Tashtiti |
|--------------|---|
| 1 | Unataka kusema nini Oscar Kwamba mimi ni dikteta? |
| 2 | Yule Musa bwana! Anataka kutupeleka Kanaani; nchi ya maziwa na asali! |
| 3 | Aa ! Bwana Oscar, naona kama umechukia vile?! |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* (2016)

Katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* msanii alionesha uongozi ambao sio wa kidikteta kwa Nyerere kumwuliza ili kuweka msisitizo Mfano “Unataka kusema nini Oscar? Kwamba mimi ni dikteta?” Haya maneno Nyerere alikuwa anayasikia lakini akauliza tena kwa ajili ya kuweka msisitizo. Nyerere ni kiongozi mzalendo mwenye uchungu na nchi yake. Nyerere alikuwa kiongozi aliyejali watu wake, alipenda ujamaa na kujitegemea na ndio maana alianzisha

mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa . Vijana wamalizapo mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa walitumikie taifa kwa moyo. Lakini Kambona alikuwa anaupenda ubepari ili wananchi waendelee kunyonywa na kunyanyaswa kwa sababu ya uongozi wa kidikteta.

Aidha msanii ameonesha jinsi Kambona alivyokuwa amekasirika kwa sababu Nyerere alimwambia habari za siasa ya ujamaa na kuapeleka vijana katika Jeshi la Kujenga Taifa baada yakumaliza vyuo na kidato cha sita. Kwa kuonesha msisistizo anasema,"Aa! Bwana Oscar naona umechukia vile? Tashtiti hii inasisitiza kwa kuonesha mtazamo uliojengwa kwa Nyerere ambaye ni mwenye msimamo na habadilikibadiliki kama kinyonga. Nyerere alikuwa kiongozi aliyesimamia haki kwa wananchi na hatimaye kuwajengea vijana uzalendo kwa kuapeleka vijana katika Jeshi la Kujenga Taifa.

4.4.8 Tanakali Sauti

Utafiti huu umechunguza na kubaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* alitumia tamathali ya semi ya tanakali sauti ili kufikisha ujumbe kwa hadhira. Hii ni tamathali ya semi inayotoa au kuiga mlion wa vitu au wanyama (Senkoro, 2011). Naye Wamitila (2010) ansema ni uigaji wa sauti fulani. Msingi mkuu wa mbinu hii ni kuhakikisha kuwa hali fulani inaelezwa kwa njia kamilifu, pia hutumiwa kujenga na kukuzia hisia fulani. Tanakali sauti ni mbinu ya kutumia maneno yanayoiga sauti au hali fulani au namna kitendo kinavyofanyika.

Msanii wa tamthiliya hii ametuonesha kuwa Nyerere hakubaliani na maandamano ya vijana wa chuo kikuu na kuamua kuwachapa viboko viongozi wa wanachuo hao.

Mfano alianza Martini ambaye alikuwa rais wa wanachuo na ndiye alikuwa mstari wa mbele kuongoza na kuratibu maandamano waliyoyafanya.

Jedwali Na 4.12: Matumizi ya baadhi ya Tanakali Sauti katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari yaKanaani

| Namba | Tanakali Sauti |
|-------|---|
| 1 | Lala chini Martini! Viboko: Chwa! Chwa! Chwa! |
| 2 | Nasema lala chini Saigoda!Viboko: Chwa! Chwa! |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka Tamthiliya ya *Nyrere na Safari ya Kanaani*(2016)

Rais Nyerere alimwamuru Martini alale chini na kuanza kumchapa viboko “Chwa! Chwa! Chwa!” Msanii amemwonesha Nyerere kuwa mwenye msimamo, anachoamua kisikilizwe na kifuatwe. Aidha mzee Mwajombe baba yake Saigoda alionesha ushirikiano wa kumlea kijana wake. Baba yake Saigoda alichukua jukumu la kumwadhibu kijana wake mbele ya Rais Nyerere na umati uliokuwa katika viwanja vya Ikulu. Vijana walitakiwa wawe na nidhamu na utiifu kwa viongozi vilevile wawe na moyo wa uzalendo wa kujenga taifa.

4.4.9 Kejeli

Mbatiah (2001) anasema kejeli ni maneno yanayotumiwa katika matamshi kwa madhumuni ya kuchoma, kukata au kutia uchungu. Utafiti ulichunguza na kubaini kuwa msanii wa tamthiliya teule alitumia kejeli kufikisha ujumbe kwa jamii. Jedwali linalofuata linaonesha ujitekezaji wa baadhi ya kejeli katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*.

Msanii alitumia kejeli katika tamthiliya hii kuwasilisha jambo la kihistoria kwa hadhira. Mfano “Ama kweli wewe Julius ni nabii Musa arap Hambiliki.” Hapa kiongozi anatakiwa abadilike awe anawasikiliza wananchi au jamii inayomzunguka.

Jedwali Na 4.13:Ujitokezaji wa Kejeli katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Kejeli |
|-------|---|
| 1 | Kama u-mwanaume kweli, bwana Bweged... |
| 2 | Ama kweli Julius ni Nabii Musa arap Hambiliki |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani (2016)

Kiongozi anatakiwa awape wananchi nafasi ya kutoa maoni kujadiliana nao ili na wao washiriki katika kuleta maendeleo ya nchi. Kejeli hiyo ilimfanya Nyerere abadilike hata pale alipoamua kuwafukuza wanachuo, baadaye aliwasamehe na kuwarudisha chuoni kuendelea na masomo yao.

4.4.10 Mdokezo

Msanii wa tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani ametumia mdokezo ili kuiwezesha hadhiara kufikiria kumalizia sentensi ambazo hazijakamilika kisanii. (Company 2008:45), wanasema mdokezo hudokeza humfanya mtu kudokeza kitu fulani na kukiacha bila kukikamilisha kwa maana ya kwamba kinaweza kukamilishwa na mtu mwingine kisanaa. Mfano “Ila nataka kusema hivi... leo...leo...,” Jedwali linalofuata utafiti ulibaini ujitokezaji wa baadhi ya mdokezo kama inavyoonekana:

Jedwali namba 4.15 linaonesha baadhi ya mdokezo ulivyotumika katika tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Mfano “Haiwezekani kama amekosa kazi yako ni kumcharaza viboko Nitamcharaza mwanangu mwenyewe mbele yako .” Msanii ametuonesha kuwa wazazi wengine

wanashirikiana na walimu kukuza maadili ya vijana wetu. Kitendo alichokifanya mzazi wa Saigoda kinatakiwa kuigwa na wazazi na jamii kwa ujumla katika kuwajengea vijana maadili na uzalendo kuanzia nyumbani.

Jedwali Na 4.14: Ujitokezaji wa Mdokezo Katika Tamthiliya ya Nyerere na *Safari yaKanaani*

| Namba | Mdokezo |
|-------|---|
| 1 | Watanzania wanakufa wakipigana na Makaburu na Mreno huko Msumbiji, Angola, Namibia, Zimbabwe, Afrika ya Kusini ...ila ninyi wendawazimu wakubwa mnasema: Afadhali wakati wa mkoloni! |
| 2 | Haiewezekani kama amekosa kazi yako ni kumcharaza viboko ... Nitamcharaza mwanangu mwenyewe mbele yako |
| 3 | Mawaziri wangu... Oscar! John! Kassim! Bibititi na wengine wote: Niseme hivi... niseme... Najaribu... Natafuta maneno mwafaka yanayoweza kulieleza hili... Kwamba nchi hii ya Tanzania ITAJENGWA NA WENYE MOYO. |
| 4 | Nimewafukuza! Mtakaa vijijini miaka mitatu...Ndiyo....! |
| 5 | Tanzania haitajengwa na ubinasi; haitajengwa kwa choyo; haitajengwa kwa tama ya kujilimbikizia mali... Wananchi; Tanzania itajengwa na wazalendo wenyewe moyo wa kuijenga Tanzania... Comrades! |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya Nyerere na *Safari ya Kanaani* (2016)

4.5 Misemo

Mtafiti katika tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani amebaini matumizi ya misemo. Wamitila (2010) anafananisha misemo na viungo ambavyo ni sawa na viungo vya upishi kwani hufanya lugha ya mwandishi huwa na mvuto mkubwa wa kisanaa. Hivyo mtafiti anaungana na Wamitila (2010) kuwa ni misemo ni fungu la maneno lililofumbata maana kimafumbo ambayo imekusudiwa kutoa funzo kwa

jamii. Kauli hizi huelezea ukweli fulani. Katika Jedwali linalofuata limewasilisha baadhi ya misemo ilijojitekeza katika tamthiliya teule.

Jedwali Na 4.15: Ujitokezaji wa Misemo katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Misemo |
|-------|--|
| 1 | Tohara ni utakaso wa mwili na roho. |
| 2 | Vitabu na maarifa ni chakula kisichoshibisha. |
| 3 | Yule daktari yuko tayari siku yoyote umwone ili aondoe hilo zu lakini wewe hutaki. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2016)

Katika utafiti huu data katika Jedwali 4.15 zinawasilishaji ujitokezaji wa misemo katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*. Msanii wa tamthiliya hii amewasilisha ujumbe wa jambo la kihistoria kwa hadhira. Mfano “Tohara ni usafi nao utakaso wa mwili na roho.” Msanii amelinganisha tohara na jeshi la kujenga Taifa. Vijana wanapoenda kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa wanapata mafunzo ya aina mbalimbali pamoja na maadili. Kwa kuwa jeshini kuna utii wa sheria na nidhamu ya hali ya juu, vijana wanaotoka huko wanakuwa wakakamavu, wenye utii na uzalendo katika nchi yao. Msanii anaposesma tohara ni usafi na utakaso wa mwili na rooho anamaanisha kijana anapomaliza kulitumika Jeshi la Kujenga Taifa, anaweza kufanya kazi za aina mbalimbali za kujitegemea.

Aidha kijana anapofanyiwa tohara anapewa mafunzo ya ujasiri na maadili jinsi ya kulinda jamii yake dhidi ya maadui na kuwa na upendo kwa watu wote. Msemo mwengine ni “Vitabu na maarifa ni chakula kisichoshibisha.” Msanii amemaanisha kujifunza hakuna mwisho. Pia msanii ameonesha kuwa binadamu anahitaji kupata

maarifa mapya kila wakati. Vijana wetu wanatakiwa wamalizapo kidato cha sita au vyuo wakaongeze maarifa zaidi juu ya mambo mabalimbali ya ujasiriamali, ukakamavu na uongozi bora wakati wakiwa katika Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo taifa litapata vijana wenye maarifa ya kutosha, wakakamavu, wabunifu na viongozi waadilifu.

4.6 Methali

Msokile (1992) anasema methali ni semi zinazotokana na ujuzi, kanuni na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri na kufundisha mambo mabalimbali kwa wanajamii. Methali hufuatilia maisha ya kila siku ya jamii kwa kujihusisha na migongano ama usuluhishi wa masuala mabalimbali katika jamii. Mulokozi (1989), oanaeleza methali kuwa ni semi fupifupi zenyenye kuelezea kwa muhtasari fikra au mafunzo yatokanayo na uzoefu wa jamii.

Methali ni maneno au sentensi zinazotolewa zenyenye mafundisho ndani yake ya kuelimisha jamii. Utafiti huu umebaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* metumia methali katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa baadhi ya methali katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*

Jedwali Na 4.16: Ujitokezaji wa Methali katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani

| Namba | Methali |
|--------------|-----------------------------------|
| 1 | Mtaka cha mvunguni sharti ainame. |
| 2 | Mvumilivu hula mbivu. |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2016)

Jedwali namba 4.16 data zimeonesha kuwa msanii wa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* ametumia methali kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mfano “Mtaka cha mvunguni sharti ainame.” Kila mtu afanye kazi kwa bidii ili aweze kupata mafanikio. Aidha ili nchi iweze kufanikiwa na kuendelea ni lazima kila mtu awajibike kwa nafasi aliyo nayo. Hivyo kila mtu aikifanya kazi kwa bidii na kuwa mzalendo kwa kujituma na kuzingatia maadili ya kazi, nchi yetu itapata maendeleo endelevu.

4.7 Nahau

Nahau ni fungu la maneno ambayo yakinangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi mfano kula mwiba maana yake kupata tabu. Tia chumvi maana yake danganya (Kamusi ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 1981). Msanii wa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* ametumia nahau kulingana na utafiti uliofanywa. Msanii ametumia nahau kwa lengo la kufikisha ujumbe alioukusudia kwa hadhira. Ujitokezaji wa baadhi ya nahau unaonekana katika jedwali linalofuata.

Jedwali Na 4.17: Ujitokezaji wa Nahau katika Tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani*

| Namba | Nahau |
|--------------|-----------------|
| 1 | Kusalimu amri. |
| 2 | Wanatia chumvi. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2016)

Msanii ametuonesha kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu walikaidi agizo la Rais liliokuwa likiwataka waende kulitumikia Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa

sheria. Na baada ya mafunzo hayo wawe wazalendo, wafuate maadili ya kazi ili walete ufanisi katika kazi. Wanachuo hawa wakaamua kuandamana ili kupinga agizo hilo. Hivyo Rais akawaadhibu kwa kuwachapa viboko viongozi wa wanachuo hao na hatimaye kuwafukuza chuo. Liboma ailikwenda kwa Martini ambaye alikuwa rais wa wanachuo na kumsisitiza kuwa wasipotimiza masharti watakuwa wamejifuta chuo.

Aidha Liboma aliwaambia Rais Nyerere akisema, amesema hata Oscar Kambona “Kasalimu amri.” Maana yake Kambona alikuwa akimpinga Rais kwa muda mrefu kwa kuwa yeye alitaka kufuata siasa za ubepari hivyo alitorokea nje ya nchi kwa kuwa uamuzi wa Rais Julius Kambarage Nyerere ulimshinda. Ilitakiwa wanachuo watii amri ya kurudi vyuoni wakamalizie masomo yao.

Tamthiliya ya *Kinjeketile*

4.8 Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

Utafiti huu ulichunguza na kubaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia tamathali za semi katika kazi yake. Msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia lugha nyepesi inayoleweka kwa urahisi na wasomaji kuliko msanii wa tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*.

Msanii wa *Kinjeketile* alitumia tamathali za semi, methali na misemo wakati msanii wa *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* alitumia nahau zaidi ya msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile*. Utafiti katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ulichambua tamathali za semi zilivyotumika na kwa kiwango gani kila moja kama jedwali linavyoonesha.

Jedwali Na 4.18: Mdafao wa Ujitokezaji wa Tamathali za Semi katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Tamatahali za Semi | Mdafao wa Ujitokezaji |
|-------|--------------------|-----------------------|
| 1. | Nidaa | 166 |
| 2. | Takriri | 54 |
| 3. | Mdokezo | 46 |
| 4. | Sitiari | 30 |
| 5. | Tashibiha | 23 |
| 6. | Kejeli | 5 |
| 7. | Tashititi | 3 |
| 8. | Tashihisi | 2 |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Utafiti ulibaini kuwa katika tamthiloiya ya *Kinjeketile* msanii alitumia tamathali ya nidaa kwa kiwango kikubwa cha mdafao wa 166, ikifuatiwa na takriri ambayo ina mdafao wa 54, mdokezo kwa mdafao wa 46, sitiari kwa mdafao wa 30. Tashibiha kwa mdafao wa 23, kejeli kwa mdafao wa 5, tashititi 3 na tashihisi kwa mdafao wa 1.

4.8.1 Nidaa

Msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia nidaa kama utafiti huu ulivyobaini katika jedwali linalofuata. Baadhi ya nidaa zilizotumika katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Msanii alitumia nidaa kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Watu walihamasisha kupigana, waweze kumwondoa mkoloni katika ardhi yao. Mfano “Sasa kupigana ! sasa vita tu, akuna jingine!” Watu hawa wamenyanyaswa na mkoloni, kiasi kwamba wamechoka wanataka uhuru wao. Kumwondoa mkoloni inatakiwa umoja wa kweli ambapo watu

hawa chini ya uongozi wa Kinjeketile waliungana na makabila ya Kusini mwa nchi yetu ili waweze kumwondoa Mjerumani.

Jedwali Na 4.19: Ujitokezaji wa Nidaa katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

| Na | Nidaa |
|-----------|---|
| 1 | Kitunda mimi nimemuona leo! |
| 2 | Sasa kupigana! Sasa vita tu, akuna jingine! |
| 3 | Wewe mwanamke ! wamatumbi waoga! |
| 5 | Tokeni! Tokeni!, wanawake wakubwa nyi! |
| 6 | Niacheni! Niacheni! mnaniumiza! niacheni niende! |
| 7 | Sote tutakuwa kitu kimoja. Maji ! |
| 8 | Nilizigusa zilikuwa kavu kabisa! |
| 9 | Umetudanganya sote ! |
| 10 | Mtanipa siku moja zaidi ! |
| 11 | Kama hatukuleta shauri, tutachelewa ! nasema –tuanze! |
| 12 | Kwanza shamba la kinoo! |
| 13 | Ua udongo mwekundu! |
| 14 | Chuki na gazabu iliyotujaa! |
| 15 | Au unaogopa! Toka mwanzo alikuwa mwoga! Yeye ni yule muongo. Kinjeketile njia moja! |
| 16 | Namimi mwenyewe nimemfundisha kushika silaha! |
| 17 | Shika silaha nikuoneshe nani anaweza kuitumia, muoga we ! |
| 18 | Si kiongozi ! Ngulumbayo tuongoze! Ndiyo tuongoze! |
| 19 | Sema ! Tuna watoto sisi. Tufikirie watoto ! |
| 20 | Nyamaza usiseme kitu! |
| 21 | Sitaki kuongea habari ya kesho! |
| 22 | Hapana ! Sitasema neno hilo! |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

4.8.2 Takriri

Utafiti huu baada ya kuchunguza na kuchambua tamthiliya ya *Kinjeketile* ulibaini kuwa takriri imetumika katika kuwasilisha ujumbe ya kazi yake kwa jamii. Takriri imetumika kama mbinu ya kuhamasisha harakati za ukombozi na kuhimiza ushujaa, mfano “ Tokeni! Tokeni!” Msanii hapa alitumia takriri ya tokeni tokeni kwa

kuwahamasisha wanachi watoke kwenda kupambana na mkoloni wasiwe waoga. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa baadhi ya takriri katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.20: Ujitokezaji wa Takriri katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Takriri |
|-------|--|
| 1 | Hodi! Hod! Fungua. Hod fungua. |
| 2 | Tokeni! Tokeni. |
| 3 | Anka! Anka!. |
| 4 | Niache!Niache! |
| 5 | Talatibu! Talatibu! |
| 6 | Nyamaza! Nyamaza! |
| 7 | Tutatambaa.Tutatambaa.Tutatambaa. Tutatambaa |
| 8 | Ua-Ua-Ua-Ua. |
| 9 | Vita! Vita! Vita! |
| 10 | Afazali kisa hiki.Afazali kisa hiki. |
| 11 | Tupo tayali! Tupo tayali! Tupo tayali! |
| 12 | Tuanze1 Tuanze! Tuanze! Tuanze! |
| 13 | Maji, Maji, Maji ya maisha ---- Maji ya maisha |
| 14 | Haifai, haifai jamaa |
| 15 | Kinjeketile muuwe! Muuwe! |

Chanzo :Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya *Kinjeketile* (2016)

Msanii wa tamthiliya hii alitumia takriri ya maji kuwajengea wananchi imani na kuwaaminisha kuwa yale maji yangewapa ushindi wa vita. Kwa imani hiyo ya maji, Kinjeketile aliweza kuwaunganisha watu wa makabila ya Kusini kupigana vita ya kumwondoa mkoloni. Mfano “Haya maji ni silaha yetu, maji ya maisha, maji haya yatamlainisha simba, maji haya yataifanya risasi kuwa chembe ya mchanga juu ya vifua vyenu”. “Ndugu tumepewa maji ndiyo, ndiyo maji tumepewa, maji ya maisha”. Watu walihamasishwa na takriri hizi ambapo msanii aliweka mkazo au msisitizo ili wananchi wa kusini wawe na imani kubwa juu ya maji ya maisha aliyo yatoa

kiongozi wao yaani Kinjeketile na ndipo wananchi walitaka ukombozi kupitia muungano wa kupigana vita kumpiga mkoloni.

4.8.3 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya semi inayotumika kuumba pitcha fulani inayotoa athari fulani au inayouumba mwitikio fulani kutoka katika hadhira. Ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu kingine. Utafiti huu uligundua kuwa msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia sitiari katika kuwasilisha ujumbe wa kazi yake. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya sitiari zilizotumika.

Jedwali Na 4.21: Ujitokezaji wa Sitiari katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Na | Sitiari |
|----|--|
| 1 | Wewe mwanamke |
| 2 | Udongo mwekundi |
| 3 | Una maana kusema mimi nitaweza kuwauzeni nyinyi nyote pamoja na watu wangu? |
| 4 | Ningelikuwa ntu wa nzungu ningelikuwa hivi? |
| 5 | Kuna moshi, naona moshi! Penye moshi pana moto kalibu kutakuwaka moto |
| 6 | Wanawake wakubwa nyie |
| 7 | Tukifika daraja hili tutakuwa kitu kimoja |
| 8 | Haya ni maji ya maisha, hii ni silaha yetu. Huu ni usinga wa nguvu |
| 9 | Usilette taa kalibu. Ondoa muangaza walisema wataleta muangaza ... kutoa giza...lakini nimetambua muangaza wao una hatali zaidi. Afazali kiza. Afazali utumwa wa mwili kuliko utumwa wa akili unaletwa na muangaza |
| 10 | Kwa nini anataka kutuuza sisi watoto wake kwa mabwana wengine? |
| 11 | Leo tumepata nguvu mpya. Leo tumepata moyo mpya |
| 12 | Wanaimba majimaji huku wamefyekwa na lisasi |
| 13 | Mala ilianza kutema lisasi |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii alitumia sitiari kuwasilisha ujumbe katika kazi yake mfano “Udongo mwekundi” Dhana ya mwandishi ni kuonesha kuwa mkoloni ni lazima aondolewe

katika ardhi ya watu wa Kusini. Mkoloni hafai katika kututawala kwa sababu anawakandamiza wananchi. Wakoloni wanapora ardhi ya wananchi, na kuwafanya wao ndio watumwa wa kuwatumikia wao. Aidha wakoloni ndio mabwana katika ardhi ya wananchi. Hiyo lazima mkoloni aondolewe katika nchi yetu, kwa kupigana vita ambapo makabila ya kuishi yaliungana na kuanza kupigana dhidi ya Mjerumani.

4.8.4 Tashibiha

Utafiti huu ulichunguza na kubainisha kuwa msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia tashibiha kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Jedwali Linalofuata linaonesha ujitokezaji wa baadhi ya tashibiha katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.22: Ujitokezaji wa Tashibiha katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Tashibiha |
|-------|--|
| 1 | Nimemuona mtu kama yeyeyeye hasa, lakini kwa mbali. |
| 2 | Sisi kama wanawake tumekaa tunatazama |
| 3 | Nimesikia habari ya bunduki inayomwaga lisasi kama mchanga |
| 4 | Afazali kufa kuliko kukaa hivi tunatawaliwa, tunalimishwa kama wanyama |
| 5 | Nnakuja kama wezi kuja kunisaidia |
| 6 | Imekuwa bahati kwenu kuwa mambo haya yametokea siku kama ya leo |
| 7 | Nendeni kama upepo kusini, kaskazini, mashariki, magharibi |
| 8 | Mbona wanitazama kama hunijui |
| 9 | Nakuona kama siye Kinjeketile |
| 10 | Na kama mibaazi tutambaa |
| 11 | Lakini ikiwa kolelo na Hongo kwa kweli ni wamoja kama wanavyosema watu wengine huko kwetu basi sisi tayari kuwa pamoja na nyinyi |
| 12 | Unafikili wale hawajui kama tumekuja |

Chanzo: Data za Utatfiti kutoka katika tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii ametuonesha jinsi wananchi walivyokuwa wakikata tamaa wakati mwingine. Mfano “sisi kama wanawake tumekaa tunantazama tu” wanaume hawa wajilinganisha na wanawake kwa vile katika jamii nyingi wanawake wanadharauliwa na hawapewi nafasi ya kutoa maamuzi katika jamii hata kama yawe maamuzi yenye tija kwa jamii. Hivyo wanaume walishindwa kuchukua hatua kwa Mjerumani ambaye alikuwa akiwanyanyasa siku zote.

4.8.5 Kejeli

Msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile*, alitumia kejeli katika kuwasilisha ujumbe wa kazi hii ya kisanii kwa hadhira kama utafiti ulivyobaini. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa kejeli katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.23: Ujitokezaji wa Kejeli kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Kejeli |
|-------|--|
| 1 | Vijitu viwili vinawatishieni –nyinyi nyote. Eti nyinyi wanaume kweli kweli wamatumbi. Hata kidogo. Wanawake tu nyinyi. |
| 2 | Mpe panya mwanamke huyu |
| 3 | Sema kama wewe mwanaume |

Chanzo: Data kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii alitumia kejeli katika tamthiliya *Kinjeketile* kuwasilisha ujumbe wa kazi yake ya kifasihi. Mfano “sema kama wewe mwanaume.” Baada ya kitendo cha kupigwa na wanyapala hadi kuishiwa nguvu, mke wake yaani Bi Kitunda aliwadharau wanaume wa jamii yao na kuwafananisha na wanawake ambao katika jamii wanadharauliwa siku zote. Hapa anatuonesha jinsi gani jamii hii ilikuwa

ikinyanyashwa na Mjerumani kwa kuwafanyisha kazi, na kuwapiga wanapodai haki zao. Kwa ujumla wananchi hawakuwa na haki katika ardhi yao hivyo ilikuwa ni lazima kumpiga Mjerumani ili kujitoa katika makucha yake. Wananchi hawa walilazimika kuungana na kuwa wamoja ili waweze kupigana na kupata uhuru wa kuishi katika nchi yao kwa amani.

4.8.6 Tashtiti

Tashititi ni mkazo wa maneno yasemwayo au yanayoandikwa ambayo yanayoweza kuwa muundo wa swali au maelezo kwa jambo linalofahamika jibu lake, lengo ni kusisitiza jambo na kuleta mshangao. Utafiti huu ulichunguza na kubaini kuwa msanii alitumia tashititi katika kufikisha ujumbe wa kazi yake ya kisanii. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa tashititi katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.24: Ujitokezaji wa Tashititi katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Tashtiti |
|-------|---------------------------|
| 1 | Eti nyinyi wanaume kweli? |
| 2 | Watu wamekufa? |
| 3 | Ujinga? Maji ujinga? |

Chanzo: Data kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia tashititi kuwasilisha ujumbe wa kazi yake ya kihistoria kwa hadhira. Mfano “Eti nyinyi wanaume kweli” swali hili wanaulizwa wanaume, ambapo jibu lake lipo. Lengo la swali ni kuweka msisitizo wa wanaume kuwa jasiri na shujaa wa kutoa maamuzi ya haraka ya kuamua kupigana vita ili kuondoa unyanyasaji waliokuwa wakifanyiwa na Majerumani.

4.8.7 Tashihisi

Utafiti huu ulichunguza na kubaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia tamathali ya tashihisi kujenga ujumbe wa kazi yake ya kisanii. Tashihisi ni tamathali ya semi ambayo sifa ya uhai huamishiwa kwenye kitu kisicho na uhai na kuvipa uwezo wa kutenda kama binadamu. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa tashihisi katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.25: Ujitokezaji wa tashihisi katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Tashihisi |
|-------|---|
| 1 | Kisasi cha siku nyingi kilituva mala moja |
| 2 | Mapenzi haya yatatuunganisha tutakuwa kitu kimoja |

Chanzo: Data kutoka katika tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii alitumia tamathali ya semi ya tashihisi kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika nchi, mfano “Mapenzi haya yatatuunganisha tutakuwa kitu kimoja “. Mapenzi yamepewa uwezo wa kuunganisha watu ili wawe na umoja. Msanii alituonesha kuwa watu wa kusini waliungana na kuwa kitu kimoja kwa lengo la kumwondoa Mjerumani ambaye alikuwa amewachosha wananchi kwa kuwanyanyasa na kuwakandamiza, na kukosa haki na uhuru katika ardhi yao.

4.8.8 Mdokezo

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* baada ya uchunguzi na uchambuzi ulibaini kuwa msanii alitumia mdokezo katika kufikisha ujumbe wa kazi yake ya kisanii. Jedwali linalofuata linawasilisha ujitokezaji wa baadhi ya mdokezo katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.26: Ujitokezaji wa Mdokezo katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Mdokezo |
|-------|--|
| 1 | Moshi ule ... Kinjeketile anafanya kafala |
| 2 | Nimemwona mtu kama yeye ... yeye hasa, lakini kwa mbali |
| 3 | Jamani mbona haludi, ntu hawesi kukaa ndani ya maji ... |
| 4 | Nilikuwa natiwa ziki ziki katika moyo wangu na jambo hili ... |
| 5 | Ondoa mwangaza ... walisema wanaleta mwangaza ... kutoa kiza ... |
| 6 | Mimi sikuleta maji, mimi ... |
| 7 | Mumetoka mbali, tumeshastahimili mengi ... |
| 8 | Tafazali kesho moja ... |
| 9 | Na kama mibaazi ... |
| 10 | Neno likintawala ntu badala ya ntu kulitawala neno ... |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* alitumia mdokezo kufikisha ujumbe kwa jamii.

Dhamira ya wananchi ni kuondoa unyanyasaji uliofanywa na mkoloni, mfano “Nzungu afukuzwe lakini kabla ya kufukuzwa” Shauku ya wananchi ilikuwa ni kupigana vita kumwondoa mkoloni, ili wapate kuishi kwa amani katika nchi yao. “Sote tunalo shauli moja lakini” Msanii ametuonesha shauri ni moja, kumwondoa mkoloni.

4.9 Methali

Baada ya uchunguzi kufanyika ulibaini kuwa msanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* ametumiamethali katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Msoikile (1992) anasema methali ni semi zinazotokana na ujuzi, kanuni na tabia za jamii ambazokwa kawaida hushauri na kufundisha mambo mbalimbali kwa wanajamii. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa methali katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.27: Ujitokeazji wa Methali katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Methali |
|-------|----------------------------|
| 1 | Halaka halakahaina balaka. |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya Knjeketile(2016)

Msanii wa tamthiliya ya Kinjeketile ameonesha msisitizo wa kuvuta subira hadi wajipange katika kumpiga Mjerumani, lakini wananchi walikuwa na haraka kwa kuwa walikuwa na maji ya maisha. Wananchi hawa walikuwa na haraka ya kupigana kwa imani ya kumshinda Mjerunmani kwa maji wailiyokuwa nayo. Kitunda anamwambia Kinjeketile “Tuanze, Tuanze,Tuanze,Tuanze!” Kwa maana kwamba waanze kupigana lakini Kinjeketile hakuwa tayari. Kinjeketile anamsihi Kitunda avute subira kwa kusema “Halaka halaka haina balaka” Msanii ameonesha msisitizo kwa jamii kupanga malengo au mambo yao vizuri kabla ya kuamua na kutofanya maamuzi ya haraka ili waweze kufanikiwa.

4.10 Misemo

Msanii wa tamthiliya *Kinjeketile* alitumia misemo kuwasilisha ujumbe aliokusudia kwa hadhira kutohana na utafiti huu ulivyobainisha. Jedwali linalofuata linaonesha ujitokezaji wa baadhi ya misemo katika tamthiliya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.28: Ujitokezaji wa misemo katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Na | Misemo |
|----|--|
| 1 | Hata kama kitu cha kula anakataa. |
| 2 | Udngo mwekundu atapigwa na atatolewa nchini. |
| 3 | Moshi kulikuwa na moshi, ukungu, kulikuwa na ukungu. |
| 4 | Afazali kisa hiki! Afazali utumwa wa mwili kuliko wa akili unaletwa na mwanga. |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii alitumia misemo katika kufikisha ujumbe wa kazi yake ya kisanii kwa jamii. Mfano “Udongo mwekundu atapigwa na atatolewa nchini,” Msanii alitumia udongo mwekundu kama mtu mbaya ambaye aliwanyanyasa wananchi. Udongo mwekundu alifananishwa na mkoloni ambaye alikuwa Mjerumani alyeitawala Kusini mwa Tanzania. Msanii aliwajengea dhamira ya kumwondoa Mjerumani ili wapate ukombozi. Wananchi walipigana kujikomboa na kupata uhuru katika nchi yao.

4.11 Kuwasilisha Dhamira kuu za Tamthiliya

Msanii alitumia vipengele mbalimbali vya lugha kuwasilisha ujumbe wa kazi za kifasihi. Katika tamthiliya ya *Nyereroe na Safari ya Kanaani*, msanii aliwasilisha dhamira kwa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama inavyoenekana katika Jedwali namba 4.32.

Jedwali Na 4.29: Ujitokezaji wa Dhamira katika Tamthiliya Teule

| Namba | Dhamira |
|--------------|------------------|
| 1 | Kujenga uzalendo |
| 2 | Demokrasia |
| 3 | Umaskini |
| 4 | Matabaka |
| 5 | Uongozi mbaya |
| 6 | Unyonyaji |
| 7 | Mapenzi |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya ya *Nyerere na safari ya kanaani* (2016)

Vipengele vya lugha katika *Nyerere na Safari ya Kanaani* vimewasilishwa na msanii na kuonesha dhamira mbalimbali zilizojiteza katika tamthiliya hii. Msanii ameonesha jinsi Nyerere alivyotaka vijana wawe wazalendo kwa kuwapeleka katika

Jeshi la Kujenga Taifa aidha ikumbukwe vijana wanapofanyiwa tohara ni sehemu ya mafunzo na maadili ya maisha. Pia aliruhusu vyama vya upinzani ili kudumisha demokrasi katika nchi. Utafiti umegundua kuwa dhamira za vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* havina tofauti kubwa na vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya ya *Kinjeketile*. Jedwali namba 4.33 linaonesha ujitokezaji wa dhamira katika tamthiliya ya *Kinjeketile*.

Jedwali Na 4.30: Ujitokezaji wa Dhamira katika Tamthiliya ya *Kinjeketile*

| Namba | Dhamira |
|-------|-------------------|
| 1 | Umaskini |
| 2 | Umoja |
| 3 | Ukombozi |
| 4 | Umaskini |
| 5 | Rushwa na usaliti |

Chanzo: Data za utafiti kutoka katika tamthiliya ya *Kinjeketile* (2016)

Msanii alitumia lugha inayozingatia vipengele vya lugha katika jedwali hapo juu kuwasilisha dhamira za tamthiliya ya *Kinjeketile*. Vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya hii vimewasilisha harakati za ukombozi na changamoto zilizowakumba. Mfano Na Mmatumbi akipigwa, Mzaramo ndiye atapiga kelele za maumivu. Hapa msanii anaonesha jinsi wananchi walivyokuwa wakihimiza umoja ili waweze kumwondoa mkoloni katika nchi yao.

Vipengele vya lugha vilevile vinaonesha jinsi wananchi walivyokuwa maskini, kwa kunyimwa ardhi ya kulima au kuchimba madini katika ardhi yao na kubaki kuwa watumwa kwa kuwafanya kazi wakoloni na kuendelea kubaki maskini. Aidha utafiti huu ulibaini kuwa vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya ya

Kinjeketile vimewasilisha dhamira. Dhamira zimewasilisha ujumbe wa kazi ya kifasihi, kuelimisha jamii, kuikosoa, kubainisha uovu na kuamsha jamii. Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* msanii ameonesha jinsi kulivyokuwa na changamoto katika maisha ya wananchi, wanapowahamasisha wenzao kwa kutoa habari kwa Mjerumani kupitia wanyapala, Hivyo kufanya umoja wao usiwe imara.” Utakachofanya askari au mnyapala kashasikia, yaani hakuna siri. Tumeshikwa na njaa, na njaa hii inatufanya tuuzane, tuna maadui na katika sisi wenyewe kuna maadui”. Katika tamthiliya hii njaa ni umaskini walionao wanachi ambao inawafanya watu wapokee rushwa na kuwasaliti wenzao.

4.12 Kulinganisha na Kulinganua Vipengele vya lugha katika Tamthiliya za

Kinjeketile na Nyerere na Safari ya Kanaani

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*, utafiti huu ulichunguza na kubaini jinsi wasanii wa tamthiliya hizi teule walivyotumia vipengele vya lugha katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii kuona kuwa wanafanana au wanatofautiana. Yafuatayo ni matokeo ya utafiti kama yalivyowasilishwa katika vipengele vifuatavyo.

4.13 Kufanana

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*, utafiti huu ulichambua na kubaini kuwa tamthiliya hizi zinafanana kimaudhui na kifani. Katika tamthiliya hizi teule zinafanana kimaudhui na kifani kwa kuwa zote wasanii wake walitumia mandhari halisi isiyo ya kubuni inayopatikana hapa Tanzania. Wasanii wa tamthiliya hizi walipangilia maneno katika sentensi kwa kuzingatia kanuni za lugha

ya kiwsahili. Aidha tamthiliya hizi zinafanana kwa kuwa zinawasilisha masuala ya kihistoria ingawaje kwa mbinu tofauti za kisanii vilevile kwa vipindi tofauti nya kihistoria.

Jedwali Na 4.31: Vipengele nya Lugha Vinavyofanana katika Tamthiliya Teule

| Na | Kipengele cha Lugha | Nyerere na Safari ya Kanaani | Kinjeketile |
|----|---------------------|------------------------------|-------------|
| 1 | Nidaa | ✓ | ✓ |
| 2 | Kejeli | ✓ | ✓ |
| 3 | Sitiari | ✓ | ✓ |
| 4 | Tashihisi | ✓ | ✓ |
| 5 | Tashibiha | ✓ | ✓ |
| 6 | Takriri | ✓ | ✓ |
| 7 | Tashtiti | ✓ | ✓ |
| 8 | Mdokezo | ✓ | ✓ |
| 9 | Misemo | ✓ | ✓ |
| 10 | Methali | ✓ | ✓ |

Tukichunguza jedwali hapo juu linaonesha kuwa wasanii wa tamthiliya teule wanafanana katika vipengele nya matumizi ya lugha. Watunzi wote wametumia vipengele nya lugha ambavyo ni tamathali za semi kama vile nidaa, kejeli, sitiari, tashihisi, tashibiha, takriri, tashtiti, mdokezo na tanakali sauti. Vilevile watunzi hawa wametumia vipengele vingine nya lugha ambavyo ni methali na misemo. Katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani msanii* amemwonesha Nyerere kuwa ni mtu mwenye msimamo kwa kusema amesimama imara kama mlima Kilimanjaro hatikisiki. Nyrerere hapa alikuwa ni mtu mwenye msimamo habadiliki na wala

hasikilizi maneno yasiyo na mwelekeo mzuri wa kuiletea nchi maendeleo. Aidha tumeona msanii wa *KinjeketileamemwoneshaKinjeketile* kuwa na msimamo wa kukataa kutawaliwa na wakoloni mfano “Afazali kufa kuliko kukaa hivi tunatawaliwa, tunalimishwa kama wanyama” Kwa kutumia nadharia ya fasihi ya jamii hii misimamo na mapambano dhidi ya mkoloni na mambo yanayotokea katika jamii unyonyaji na rushwa yanahifadhiwa na kubaki kuwa historia.

4.14 Kutofautiana

Jedwali Na 4.32: Vipengele vya Lugha Vinavyotofautiana katika Tamthiliya Teule

| Namba | Kipengele cha lugha | <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> | <i>Kinjeketile</i> |
|----------|---------------------|-------------------------------------|--------------------|
| 1 | Tanakali sauti | ✓ | ✗ |
| 2 | Nahau | ✓ | ✗ |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya teule (2016)

Tukichunguza jedwali hapo juu linaonesha kuwa wasanii wa tamthiliya teule wametofautiana katika matumizi ya vipengele vya lugha. Msanii wa tamthiliya *Nyerere na Safari ya Kanaani* ametumia kipengele cha lugha cha tamathali ya semiya tanakali sauti wakati msanii wa *Kinjeketile* hajatumia kipengele hicho. Aidha msanii wa Nyerere na Safari ya Kanaani ametumia kipengele cha lugha nahau lakini msanii wa *Kinjeketile* hakutumia. Kwa hiyo msanii wa tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* Mbogo ametumia vipengele vya lugha vine ambavyo ni tamathali za semi, misemo, methali na nahau wakati msanii wa *Kinjeketile* Hussein ametumia vipengele vitatu vya lugha ambavyo ni tamathali za semi, misemo na methali

4.15 Kufanana au Kutofautiana kwa Dhamira Zilizojitokeza katika Tamthiliya Teule

Tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* zimetungwa kwa umahiri, katika kujadili masuala ya kihistoria yaliyojitokeza katika jamii.

Jedwali Na 4.33: Kufanana kwa Dhamira Zilizowasilishwa na Vipengele vya Lugha

| Namba | Dhamira | <i>Kinjeketile</i> | <i>Nyerere na Safari ya Kanaani</i> |
|--------------|--------------------|---------------------------|--|
| 1 | Matabaka | ✓ | ✓ |
| 2 | Umaskini | ✓ | ✓ |
| 3 | Nafasi ya mwanamke | ✓ | ✓ |
| 4 | Uongozi mbaya | ✓ | ✓ |
| 5 | Rushwa | ✓ | x |
| 6 | Mapenzi | x | ✓ |
| 7 | Ukombozi | ✓ | x |

4.15.1 Matabaka

Wasanii wa tamthiliya ya *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* walionesha dhamira ya matabaka. Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* msanii alionesa matabaka pale Mjerumani alipowagawa watu. Kuna Mjerumani (mkoloni) ambaye alikuwa na maisha ya hali ya juu, halafu mnyapala ambaye yeye ndiye anayesimamia wenzake wafanye kazi na wale wanaotumikishwa na Mjerumani. Hivyo hapa kulikuwa na tabaka la mabwana na watumwa. Katika tamthiliya ya *Nyerere na Safari ya Kanaani* kulikuwa na tabaka la matajiri na la maskini kwa sababu baada ya kupata uhuru miaka michache watu walianza kujilimbikizia mali na kuwa matajiri. Ndipo lilipotokea tabaka la matajiri na maskini.

4.15.2 Uongozi Mbaya

Msanii katika tamthiliya ya Kinjeketile alionesa uongozi mbaya pale ambapo Kinjeketile aliwapa wananchi maji ya kujilinda wakati wa vita lakini akawa hatoi maamuzi ya kupigana na Mjerumani. Katika Tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani msanii alionesa uongozi mbaya pale wanafunzi wa vyuo vikuu walipotaka kuzungumza na Rais kwa ajili ya suala la Jeshi la Kujenga Taifa na kukatwa asilimia 60% ya mshahara kwa muda wa miezi 18 watakapoajiriwa. Rais Nyerere alikataa kukutana nao na kusikiliza maoni yao ndipo walipoamua kuandamana na kubeba mabango yenyе malalamiko yao hadi viwanja vya Ikulu.

4.15.3 Nafasi ya Mwanamke

Katika tamthiliya zote mbili nafasi ya mwanamke imebainishwa. Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* msanii amemwonesha mwanamke kama ni mtu tegemezi. Mwanamke alimtegemea mume wake kwa kila hali hata pale ambapo waume zao walienda kufanya kazi kwa Mjerumani wao, walikuwa wanasubiri bila kufanya kazi na mwishoni tatizo la njaa likajitokeza.

Katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari yaKanaani* msanii amemwonesha Farida kuwa na uamuzi wa kumchagua mchumba wake mwenyewe. Baba yake Farida alikuwa hampendi Martini kwa sababu alikuwa hajafanyiwa tohara. Zebedayo baba yake Farida alikuwa amesikitika kwa sababu ya msimamo wa Farida wa kutaka kuolewa na Martini. Mfano Zebedayo alisema “Niko katikati ya bahari machafukoge. Milima ya mawimbi ya bahari karibu kunizika. Siliioni tumaini la kumwepusha binti yangu Farida dhidi ya hii nakama.

4.15.4 Umaskini

Msanii katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ameonesha umaskini uliosababishwa na wakoloni. Wakoloni hawa walichukua wananchi kwenda kuwalimia mashamba na kazi mbalimbali. Wakati walipokuwa wakifanya kazi kwa wakoloni, walishindwa kuzalisha mali kwa ajili ya familia zao. Kwa hiyo uzalishaji kwa ajili ya familia ulikuwa ni kidogo hivyo kupelekea wanachi kuwa maskini kwa kukosa chakula na mahitaji yao mbalimbali.

Katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* msanii ametuonesha Martini alipowasilisha umaskini, alipokuwa akisoma risala mbele ya Rais Nyerere baada ya maandamano. Alisema wazazi wao ni maskini na wanawategemea wao wasome wapate kazi ndipo wakawasaidie. Badala yake serikali inawaambia baada ya kumaliza vyuo ni lazima walitumikie Jeshi la Kujenga Taifa kwa wa miezi sita. Na watakapoajiriwa kazi wakatwe asilimia sitini ya mshahara kwa muda wa miezi kumi na nane.

Jedwali Na 4.34: Kutofautiana kwa Dhamira zilizowasilishwa na Vipengele vya Lugha

| Namba | Dhamira | <i>Nyerere na Safari ya Knaani</i> | <i>Kinjeketile</i> |
|-------|-------------------|------------------------------------|--------------------|
| 1 | Rushwa na Usaliti | ✗ | |
| 2 | Mapenzi | ✓ | ✗ |
| 3 | Ukombozi | ✗ | |

Chanzo: Data za Utafiti kutoka katika Tamthiliya teule (2016)

4.15.5 Rushwa na Usaliti

Katika Jedwali namba 4.37 kujitokeza kwa dhamira kumetofautiana. Rushwa na usaliti vimejitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* wakati katika tamthiliya ya

Nyerere na Safari ya Kanaani hakuna. Wananchi wao kwa wao wanatoa sirina kuwasaliti wenzao ambapo inapelekea umoja waokukosa nguvu na wakati mwingine adui amekuwa akipata siri zao na hii inawapelekea kutokushinda vita kwa urahisi.

4.15.6 Mapenzi

Katika tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani msanii aliongelea mapenzi ya Farida na Martini ambayo hayakuwa ya siri. Wawili hawa walipendana kwa dhati. Martini alikuwa hajafanyiwa tohara lakini kwa kuwa Farida alikuwa na mapenzi ya dhati kwake alimhimiza atahiriwe ili waweze kutimiza ndoto yao ya kuoana. Hata pale walipofanya maandamano na Rais Nyerere akawafuza chuo waliendelea na mapeni yao. Walipokuwa kijijini kwao Martini alitahiriwa kwa nguvu bado aliendelea kumhudumia na baadaye walirudi chuoni kumalizia mafunzo yao.

4.15.7 Ukombozi

Katika tamthiliya ya Kinjeketile msanii ameonesha harakati za mapinduzi na ukombozi zilizofanywa na wananchi wa Kusini mwa Tanzania. Wananchi hawa walipambana na Mjerumani ili kumwondoa katika nchi yao. Katika tamthiliya ya Nyerere na Safari ya Kanaani mkoloni alikwishaondolewa na dhamira ya ukombozi hapa haipo. Kilichokuwepo Nyerere alikuwa anajenga jamii mpya isiyokuwa na wanyonyaji wanaojilimbikizia mali na kujenga matabaka katika jamii ya walio nacho na wasokuwa nacho.

4.15.8 Hitimisho

Sura hii imejadili data za matokeo yaliyopatikana kulingana na malengo mahsus ya utafiti huu. Mtafiti ameonesha vipengele vya lugha ambavyo vimetumika katika tamthiliya teule.

Aidha utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya ya *Kinjeketile* imetumia lugha ya kawaida inayomwezesha msomaji kuelewa kwa urahisi ujumbe wa kihistoria uliowasilishwa na msanii. Vilevile utafiti umebainikuwa tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* zimetumia vipengele vya lugha ambavyo vimetumia lugha ya kitamathali zaidi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira. Vipengele vya lugha vilivyotumika katika tamthiliya teule vimeeleza kuwasilisha dhamira kuu za tamthiliya hizo, ambazo ni harakati za ukombozi na mapinduzi, nafasi ya mwanamke, unyonyaji na ukandamizaji, rushwa na usaliti. Tamthiliya teule zinawasilisha suala la kihistoria kwa vipindi viwili tofauti, *Kinjeketile* imewasilisha harakati za watu wa Kusini mwa Tanzania katika kupambana na mkoloni kabla ya uhuru. Watu hawa wa Kusini waliamini kuwa risasi zitageuka kuwa na wao maji na wao kupata ushindi kwa urahisi. Tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* imewasilisha historia ya nchi baada ya uhuru ambapo imejadili harakati za kupambana na ukoloni mambo leo. Tanzania baada ya uhuru, kwa muda mfupi watu walijilimbikizia mali na kujenga tabaka la matajiri na maskini, ambapo Rais Nyerere hakukubaliana na jambo hilo. Sura inayofuata inawaslisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho hutoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti uliofanyika. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo, sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho na sehemu ya tatu inahusu mapendekezo ya utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti ulilenga kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya za kihistoria za *Kinjeketile* iliyoandikwa na Ebrahim Hussein na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Lengo ni kutaka kuibua matumizi ya lugha na vipengele vyake na dhamira vilivytumika katika kuwasilisha ujumbe katika jamii na kuvilinganisha kutoka kwa msanii mmoja na mwengine. Tatizo la utafiti huu ni kutathmini vipengele vya lugha na dhamira katika tamthiliya teule ili kuweza kuona jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizi wanafanana au kutofautiana.

Lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza. Ilikuwa ni kutathmini vipengele vya lugha kwa kulinganisha tamthiliya ili kubaini vipengele vinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa tamthiliya hizi. Malengo mahsus ya utafiti huu yalikuwa : Kutathmini matumizi ya lugha na dhamira katika tamthiliya teule na kulinganisha na kulinganua uteuzi wa vipengele vya lugha katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Ili kufikia malengo hayo utafiti huu ulikusudia kujibu maswali haya yafuatayo: Je, ni vipengele vipi vya lugha vilivyojitokeza katika

tamthiliya hizi? Uteuzi wa vipengele vya lugha katika tamthiliya teule unafananana au kutofautiana kwa vipi katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii? Ni dhamira zipe zilizojitokeza katika tamthiliya teule? Uteuzi wa dhamira katika tamthiliya teule unafananana au kutofautiana kwa vipi katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii? Kuna tafiti nyingi zilizofanywa za kulinganisha kazi za tamthiliya lakini ulinganishaji huo haukuzingatia masuala ya kihistoria. Aidha tafiti nyingi zilijikita kulinganisha fani na maudhui ya kazi za fasihi. Utafiti unahitajika kufanyika juu ya kutafiti jinsi matumizi ya lugha na dhamira vinavyoweza kumtofautisha msanii mmoja na msanii mwingine, pengo ambalo utafiti huu umekusudia kuliziba.

Kulingana na malengo ya utafiti huu, nadharia ya fasihi ya jamii ndiyo iliyotumika na kuongoza katika kuchunguza na kuchambua data za utafiti huu. Utafiti ulikusanya data kwa kusoma machapisho katika maktaba. Mbinu hii ya usomaji katika maktaba ilisaidia kuchambua vitabu vyote viwili na kubainisha matumizi yalugha na vipengele vyake na dhamira zilizojitokeza. Wananchi au wasomaji waliweza kuelimika kupitia masuala ya historia yaliyowasilishwa na wasanii wa tamthiliya hizi.

Baada ya utafiti imebainika kuwa wasanii wa tamthiliya teule wametumia vipengele vya lugha kuwasilisha ujumbe kwa jamii ambavyo ni methali, nahau, misemo na tamathali za semi. Baadhi ya tamathali za semi ni kama sitiari, kejeli, mdokezo, tashibiha, takriri, tashihisi, nakadhalika. Vipengele vya lugha vilivytumika vinamtofautisha msanii wa tamthiliya moja na tamthiliya nyingine. Katika kujibu swalii la kwanza la utafiti huu ni kuwa utafiti ulichunguza matumizi ya lugha katika tamthiliya ya *Kinjeketile*. Utafiti uligundua kuwa msanii alitumia lugha rahisi

inayomwezesha msomaji kuelewa kwa urahisi. Tamathali za semi zilitumika ambazo ni sitiari, tashibiha , tashihisi, takriri, kejeli, tashtiti, na nidaa. Utafiti ulichambua na kugundua kuwa tamthiliya ya *Kinjeketile* ambayo imeawasilisha masuala ya historia ya tukio ambalo lilitokea kwa wananchi wa Kusini mwa Tanzania. Wananchi wa Kusini walipigana vita kumwondoa Mjerumani na utawala wake.

Aidha katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* msanii alitumia vipengele vya lugha ambayo ni pamoja na methali, nahau, misemo na tamathali za semi ambazo ni sitiari, tashihisi, tashibiha, tashtiti, na takriri. Matumizi haya ya lugha na vipengele vyake ambavyo msanii alitumia kwa lengo la kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Wasomaji wakisoma tamthiliya hii waweze kujuwa kwamba kumbe kulikuwa na tohara na Jeshi la Kujenga Taifa katika jamii iliyokuwepo awali. Data za utafiti huu zilizokusanywa, zimechambuliwa kwa uchambuzi linganishi. Katika kujibu swalii la pili la utafiti huu ambalo lililenga kubainisha matumizi ya lugha na vipengele vyake vinafanana au kutofautiana kwa vipi katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii katika tamthiliya teule. Utafiti huu ulibaini dhamira zilizojitokeza katika jamii na kufikisha ujumbe katika jamii. Hivyo vipengele vya lugha katika tamthiliya hizi zinaelimisha, kukosoa na kuamsha jamii. Katika dhamira, vipengele vya lugha vimetumika kujenga jamii katika kazi za fasihi. Kwa mfano nafasi ya mwanamke, harakakati za ukombozi, uongozi mbaya, rushwa, imani za jadi na usaliti.

Kujibiwa kwa swalii la nne ni kutokana na data zilizopatikana katika utafiti kama ifuatavyo: Ni kulinganisha na kulinganua dhamira na jinsi zilivyotumika na wasanii wa tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere na Safari yaKanaani* katika kuwasilisha ujumbe katika jamii husika. Utafiti ulibaini kuwa katika uteuzi wa vipengele vya

lugha wasanii wa tamthiliya hizi wametofautiana. Tamthiliya hizi zinatofautiana katika uteuzi wa matumizi ya vipengele vya lugha. Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* msanii alitumia lugha ya kawaida inayomwezesha msomaji kuelewa ujumbe uliopo kwa urahisi. Kwa mfano “Wewe mwanamke, Wamatumbi waoga! Sisi sote tunataka Mjerumani aondoke.” Katika mifano hiyo lugha iliyotumika iko wazi, msomaji anaewa ujumbe uliopo moja kwa moja. Tofauti ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* ambapo msanii ametumia lugha ambayo msomaji ni lazima afikirie ili kupata wazo la msanii. Mfano “Tohara ni roketi” Hapa lazima msomaji atafakari ili aweze kupata wazo au dhamira ya mtunzi ndipo apate ujumbe uliopo.

Katika utafiti huu ulibaini kuwa mbinu za matumizi ya lugha ambazo zinatofautisha tamthiliya hizi katika kiwango cha utumizi na kubainisha upekee wa msanii kutokana na athari za kimazingira na kihistoria. Kwa mfano katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ni tamthiliya iliyojikita katika utunzi wa kiaristotle, kwa sababu inazungumzia juu ya mhusika mkuu ambaye aliaminiwa na watu na baadaye kupata anguko. Katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaanimsanii* ameonesha suala la kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa kama mafunzo katika jamii. Kwa hiyo msanii wa *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* amejikuta akitumia zaidi vipengele vya lugha kuliko *Kinjeketile*.

Kufanana kwa tamthiliya hizi ni kwa sababu zote zinawasilisha masuala ya kihistoria ingawa ni mbinu tofauti za kisanaa na vipindi tofauti vya kihistoria. Hivyo inakuwa vigumu kutoa hitimisho kuwa tamthiliya hizi za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* zinafanana.Utafiti huu uligundua kufanana kwa tamthiliya hizi katika matumizi ya tashihisi,tashibiha, tashtiti, sitiari, takriri, kejeli na mdokezo. Pia kufanana kwa tamthiliya hizi ni katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa kutumia

vipengele vya lugha. Mfano wa dhmira hizo ni uongozi mbaya, umaskini, matabakana nafasi ya mwanmke. Wasanii wa tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* wanafanana kwa kuwa wametoka jamii zenyе historia zinazofanana, itikadi moja, siasa na zinafanana kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Kutofautiana kwa tamthiliya hizi msanii wa tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* ametumia vipengele vinne vya lugha ambavyo ni tamathali za semi, methali misemo na nahau wakati msanii wa *Kinjeketile* ametumia vipengele vitatu vya lugha navyo ni tamathali za semi, methali na misemo. Katika tamathali za semi msanii wa *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* ametumia tanakali sauti ambapo *Kinjeketile* hakutumia. Kutofautiana kwa dhamira zilizojitokeza *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* kuna mapenzi ya Farida ambaye alimpenda Martini kwa dhati wakati Martini alikuwa hajatahiriwa lakini katika tamthiliya ya *Kinjeketile* mapenzi hayapo. Dhamira za rushwa na ukombozi zilijitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* wakati katika *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* hazikujitokeza. Wanachi wa Kusini walipambana na mkoloni ili kjikomboa kutoka katika makucha yao ya kunyanyaswa.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu umejadili matumizi lugha na vipengele vyake na dhamira zilizojitokeza zilivyotumika katika tamthiliya zilizochunguzwa za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani*. Katika utafiti huu uamebaini kuwa tamthiliya *Knjeketile* imetumia vipengele vya lugha ambavyo ni pamoja na tamathali za semi, methali, na misemo. Aidha msanii wa tamthiliya hii ametumia lugha ya kawaida na ya wazi ambayo inamrahisishia msomaji kuelewa au kupata ujumbe uliowasilishwa.

Katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* utafiti umebaini kuwa msanii ametumia vipengele vya lugha ambavyo vimebebw na lugha zaidi ya *Kinjeketile*. Vipengele hivyo vya lugha ni kama vile tamathali za semi, methali, nahau na misemo. Hivyo utafiti umebaini kuwa tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* imetumia lugha ya kitamathali zaidi katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Pia msanii ametumia lugha inayomfikirisha msomaji ili aweze kubaini ujumbe uliokusudiwa. Utafiti umebaini kuwa tamthiliya hizi zinatofautiana katika kuwasilisha suala la kihistoria, kwa kuwa wasanii hawa wanawasilisha historia ya jamii kwa muda tofauti.

Msanii wa *Kinjeketile* amejadili kwa uhalisia juu ya jamii ya Kusini kabla ya uhuru, katika kupambana kwa kupigana vita na Mjerumani. Watu wa Kusini waliamini kuwa maji yanaweza kubadili risasi kuwa maji na kuweza kumwondoa Mjerumani katika ardhi yao. Aidha katika tamthiliya ya *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* msanii amewasilisha historia katika kipindi baada ya uhuru, hivyo kujadili historia ya harakati za kujenga ujamaa na uzalendo baada ya wakoloni kuondoka.

Wasanii wa Tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* wanafanana kwa ujumbe wa kazi zao kwa kuwa wamejadili mambo yaliyopo katika jamii kama vile harakati za ukombozi, rushwa, usaliti, na nafasi ya mwanamke. Pia wamejadili vipengele vya lugha katika tamthiliya teule. Aidha utafiti umebaini kuwa tamthiliya hizi zimeandikwa na wasanii wa jamii moja ambao walishuhudia na kupata masimulizi ya historia ya jamii yao. Hivyo wanafanana katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

Utafiti huu umeleta faida kwa taaluma ya fasihi kwa wasomi kwani utatajirisha maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Wanachuo watakaosoma utafiti huu watapata rejea ya mambo mbalimbali ya kimtindo na wengine watatumia kwa kuandika katika tangulizi ya kazi zao. Pili utafiti huu umetoa mchango wake kwa jamii umuhimu wa historia ya nchi au jamii, ni kwa namna gani kazi za fasihi zinavyobeba historia ya nchi. Tatu, utafiti huu umesaidia kukuza lugha kwa kuva vipengele vyake vimefanuliwa namna viliviyotumika katika kazi hizi, za kifasihi kama matumizi ya tamthali za semi, methali, nahau na misemo. Hivyo kuwafanya watakaosoma kazi hizi kukuza msamiati na uwezo wa kutumia lugha kisanaa. Nne, utafiti huu utachochea ari ya tafiti tofauti tofauti za kifasihi zikiwemo tamthiliya za Kiswahili hasa zile zinazozungumzia historia fulani ya nchi au jamii.

5.4 Mapendekezo

Tamthiliya za *Kinjeketile* na *Nyerere* na *Safari ya Kanaani* zimewasilisha suala la kihistoria kwa nyakati mbili tofauti. Utafiti umeweza kizilinganisha tamthiliya hizi na kuonesha zinavyotofautiana katika uteuzi wa vipengele vyta lugha. Utafiti huu unapendekeza kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa hali ya juu kabisa juu ya kazi nyingine zilizoandikwa juu ya historia ya nchi au jamii. Pia unapendekeza watatafiti wajitokeze katika kufanya utafiti unaohusu kazi za kisanaa za kihistoria. Wasanii wajitokeze katika kutunga kazi za fasihi zinazobeba historia ya nchi au jamii hasa tamthiliya za Kiswahili. Aidha tafiti mbalimbali ziendelee kufanyika ambapo zitakuza matumizi ya lugha na kuibua dhamira ili kuwawezesha wanachuo kupata rejea ya kazi zao.

MAREJELEO

- Alderson, C. G. & Berretta, A. (1992). (Wah.) *Evaluating Second Education: Cambridge Applied Linguistics*. London: Cambridge University Press.
- Bachman, R., & Schutt,R. (2007). *The Practice of Researchin Criminology and Criminal Justice*(Toleo la 3). London: Sage Publications Inc.
- Baker, T. (1994). *Doing social research*. Singapore: McGrwa-Hill.
- Bakiza, (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasihi*. Nairobi: Oxford University Press East Africa, Ltd.
- Basnell, S. (1993), *Comparative Literature: A Critical Introduction*, Oxford: Blackwell.
- Berg, B. L. (2004). *Qualitative Research Methods for the Social Science*. (Toleo la 5.). Boston: Pearson Education, Inc.
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*. (Toleo la 2) Oxford: Oxford Univerity Press.
- Best, J. W., & Kahn, J. (1993). *Research in Education*. New York: Allyn Bacon Inc.
- Cohen, L, Manion, L., & Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education*. (Toleo la 5). London: Rutledge Falmer.
- Corbetta, P. (2003). *Social Research: Theory, Methods and Techniques*. London: Sage Publications Inc.
- Crystal, D., & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Green and Co. Limited.
- Cuddon, J. A. (1998). *Dictionary of Literarry Terms and Literary Theory*.London: Blackwell Publishers Ltd.

- De Vaus, D. A. (1993). *Surveys in Social Research* (Toleo la 3.). London:University College London Press.
- De Vaus, D. (1985). *Surveys in Social Research*. (Toleo la 5.). London: Routledge.
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Cambridge: Blackwell.
- Escarpit, R. (1974). *Sociology of Literature*. London: Frank Cass and Co. Ltd.
- Hollway, L. (1997). *Basic Concepts for Qualitative Research*. Oxford:Blackwell Science.
- Hussein, E. (2003). “Hatua mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthiliya Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle.” Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111 FASIHI*. TUKI. Dar es Salaam.
- Hussein, E. (1969), *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi*, Dar es Salaam, Daud Publish Company.
- Kahigi, K. K. (1995). *Kioo cha Lugha:Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Kiango, S. D. (1980). “*Tamthiliya ya Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira 1957 - 1975*” *Tasnifu ya Umahiri*.,Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiango, S. D. (1982), “*Tamthiliya ya Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa,*” *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*.Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiango, S. D. (1990). “*Mwelekeo wa Tamthiliya za Kiswahili.*” *Jarida la Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- King'ei, J. K. (1987). "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Hussein." *Katika Mulika*. 19, 19- 35.
- King'ei, K., na Catherine, N. M (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kombo, D. K., & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and ThesisWriting: Introduction*, Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. K. (1990), *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Willey Eastern Ltd.
- Kothari, C. R. (1993). *Research Methods : Methods and Techniques (Toleo la 2)*. New Delhi: Willey Eastern Ltd.
- Kvale, S. (1996). *Interviews An Introduction to QualitativeResearch Interviewing*. London: Sage Publications Inc.
- Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*.Chicago: University of Chicago Press.
- Lakoff, G. & Johnson, M. (1988), *Metaphors we Live By (Toleo la 2)*: Chicago: Chicago University Press.
- Lee, R. M. (1993). *Doing Research on Sensitive Topics*. London: Sage Publications Inc.
- Mahenge, E. (2014). *Nelson Mandela*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.
- Mauya, A. B. (2006). *Semi Maan na Matumizi*. Dar es Salaam: Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Maxwell, J. A. (2005). *Qualitative Research Design: An Interactive Approach*. London: Sage Publications Inc.

- Mazrui, A. M., & Syambo, B. K. (1992), *Uchambuzi wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Mbogo, E. (1993). “*Matumizi ya Dhana na sanaa katika Sanaa za Maonesho za Jadi katika Tamthiliya ya Leo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mbogo, E. (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaani*, Dar es Salaam: Karljamer Print Tecnilogy.
- Mlacha, S. A. K. (1981). *Methali kama Chombo Muhimu katika Jamii*, Makala za Dar es Salaam: TUKI.
- Mlama, P. O. (2003). “Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania,” *Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III FASIHI*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msanjila, Y. P. Kihore, Y. M., na Massamba, D. P. B. (2010). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi fupi*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mugenda, O. M., na Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press Kenya.
- Mulokozi, M. M., na Kahigi, K. K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Mulika namba 21. Dar es Salaam: TUKI.

- Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dares Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Mutembei, K. A. (2012). *Korasi katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Taaluma ya Taasisi za Kiswahili. Daar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es laam.
- Mutembei, K. A. (1997). "Korasi na Uhusiano Wake na Sanaa za Maonesho: Uchambuzi wa Kidaikronia" *Katika Kioo cha Lugha Juzu*. 1(2), 67 – 72.
- Mutembei, K. A. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K., na Chimerah, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Nkwera, F. V. (1979). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods ni Social Work Research; Challenges and Rewards*. London: Sage Publications Inc.
- Patton, M. (2002). *Qualitative Research and Evaluation Method* (Toleo la 3). London: Sage Publications.
- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*, Nairobi: Karljamer Print Tecnology.
- Powell, R. R., & Lynn, S. C. (2004). *Basic Research Methods for Librarian*. (Toleo la 5.). London: Sage Publications Inc.
- Punch, K. F. (2005). *Introduction to Social Research: Qualitative and Quantitative Approaches*. (Toleo la 2.). London: Sage Publications Inc.

- Ramadhan, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo's Ngoma ya Ngw'anamalundi and Hussein's Morani. A Stylistic Comparison.* Tasnifu ya Umahiri. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Richard, M. N. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Schutt, R. K. (2006). *Investigating the Social World: The Process and Practice of Research.* London: Sage Publications Inc.
- Semzaba, E. (2003). *Tamthiliya ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam. Tanzania.
- Sengo, T. S. Y. (2008). *Sengo na Fasihi za Kinchi,* Dar es Salaam: AERA Publishers.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research: A Practical Handbook* (Toleo 2.). London: Sage Publicatins Inc.
- Totosy de Zepetnek, S. (1996a). "Essays in Reader-Oriented Theory, Criticism, And Pedagogy," Katika jarida la *International Pesrspectives onReading*, Mh. Steven Totosy de Zepetnek, Michigan Tecnological University, Michigan.
- Totosy de Zepetnek, S. (1996b). "Thematic Cluster Canadian Review of Comparative Literature," katika jarida la *Comparative Literature: History and Contemporaneity*, juzuu ya *Utangulizi wa Fasihi Linganishi.*
- TUKI, (2004). *Kamus ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Wallek, R., na Warren, A. (1948). *Theory of Literature*, Harcourt, Brace and Company. New York.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.
- Wamitila, K. W. (2010), *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.
- Wamitila, K. W. (2010), *Kichocheo cha fasihi, Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, W. K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Weiss, R. S. (1994). *Learning from strangers: The art and method of qualitative interviewing*. New York: Free Press.